# Mkataba Adhimu Wa Kulingania

**Mwandishi: Hisham Al Talib**

**Mfasiri: Badru Jaffar Swaleh**

Daktari Hisham Yahya Al Talib alizaliwa nchi ya Iraq mwaka 1940. Alitunukiwa shahada ya kwanza ya uhandisi wa umeme kutoka Chuo Kikuu cha Liverpool nchini Uingereza mwaka 1962 na shahada ya udaktari ya uhandisi wa umeme kutoka Chuo Kikuu cha Purdue, Indiana Amerika mwaka 1974.

Alijiunga na shughuli za kuhudumia Uislamu nchini Amerika Kaskazini wakati akisoma na ameendelea kuuhudumia Uislamu hadi sasa. Amehudumu katika nyadhifa mbalimbali katika vyama tofauti vya Kiislamu, miongoni mwa nyadhifa hizi ni; ukurugenzi wa kitengo cha mafunzo ya uongozi katika Chama cha Wanafunzi wa Kiislamu nchini Canada na Amerika (1975-1977), katibu mkuu wa Umoja wa vyama vya wanafunzi wa Kiislamu ulimwenguni (1976). Pia amesimamia na kufundisha mfululizo wa mafundisho ya uongozi na kongamano za kielimu Amerika Kaskazini na kwengineko.

Daktari Hisham Altalib ni mwanzilishi wa Taasisi ya Kitaifa ya Fikra ya Kiislamu (1981) (International Institute of Islamic Thought). Pia Daktari Hisham alikuwa mwanachama muanzilishi wa Taasisi ya Misaada ya Saar (Saar Foundation) (1983-1995). Ameandika kitabu mashuhuri ‘*Dalēl At-tadrēb Alqiyādy*’ ‘Dalili ya Mafunzo kwa Watumishi wa Uislamu’ kilichofasiriwa kwa lugha zaidi ya ishirini. Kwa sasa Daktari Hisham ni mkufunzi wa idara ya fedha katika Taasisi ya Kitaifa ya Fikra ya Kiislamu mji mkuu wa Washington.

# Mkataba Adhimu Wa Kulingania

Daktari Hisham Al Talib

## Fikra ya Mkataba

Mkataba huu ni mwito kwa Waislamu kwa jumla na walinganizi (mada'i) hasa kuungana pamoja na kushikamana na misingi, misimamo na miondoko maalum. Kushikamana na jumla ya misingi hii utabuni mkataba adhimu wa kulingania, na njia za kuimarisha fikra na utendakazi. Natija ya mwendo huu ni kupatikana mafanikio makubwa, kusibu ukweli, kuhamasika na kupungua hitilafu, makosa na tofauti baina ya walinganizi na kuacha kutokushughulika na da'wa.

## Utangulizi

Ulimwengu wa Uislamu unapitia mwamko wa kina. Tukio hili na mwelekeo huu mzuri wa baraka ni ishara ya kutanabahi kwa Umma wa Kiislamu, kuzinduka kwake kutoka usingizini, kujitambua, kujifahiri na dini yake, kujitahidi kuenda mbele, kujikomboa kutokana na hali ya kutegemea fikra na mifumo isiyokuwa ya Kiislamu. Mwamko huu ndio unaoashiriwa kwa lahja ya kisasa kama '*As sahwa Al islāmiya'* (Mwamko wa Kiislamu).

Allah aliyetukuka – shukrani na fadhila zote zarejea kwake – ameafikisha mwamko huu kufikia nchi zisizokuwa za Kiislamu, nchi zilizo na idadi chache ya Waislamu waliohamia huko kwa ajili ya kazi au masomo. Miongoni mwa mambo ya kushukuriwa kuhusu Waislamu wanaoishi nchi hizo, hasa katika miaka ya karibu ni kuunda vyama ili kuuhudumia Uislamu kwa nidhamu na mpangilio. Taasisi hizi zilichukua mwongozo kutoka kwenye vitabu vya *fikihi* kwa mambo ya kidini na ya kidunia, vilevile zilitegemea mwongozo wa kiidara katika vitabu vya idara ili kusuluhisha makosa ya kiidara na kuweka mikakati madhubuti ya kuepukana na makosa hayo. Taasisi hizi ziliwakilisha Uislamu na Waislamu serikalini, jambo hili lilikuwa hatua kubwa, kwani Waislamu waliohamia nchi za Magharibi walipevuka akili na kuondoa fikra za uanafunzi, ugeni au ufanyikazi; yaani wapita njia. Waislamu hawa, pamoja na umahiri na juhudi waliokua nazo walikuwa na nishati zisizokuwa na mpangilio, na uwezo wao ulikuwa finyu. Ingawa juhudi zao zilikuwa nzuri, hawakupata athari kubwa wala zenye kuvutia.

### Dalili za Mwamko

Mwamko huu wa Waislamu uliobarikiwa umedhihiri kwa sura mbalimbali na kutofautiana nchi hadi nyengine kuambatana na hali zilizowazingira Waislamu. Kwa baadhi ya Waislamu umedhihiri kwa taasisi za Kiislamu au msikiti, au shirika la kibiashara, au taasisi za fedha kama vile benki, au miradi ya kuwasaidia maskini kwa mikopo, au jarida au gazeti, au uandhishi wa vitabu au kufasiri vitabu na kuvisambaza, au mlinganizi (mwalimu au imamu) aliyetumwa kutoka nchi fulani au kikundi kinachotetea na kupigania kusimamisha Sheria za Kiislamu katika nchi ya Waislamu au harakati za kukomboa nchi ya Waislamu kutokana na ukoloni na kadhalika.

Ingawa mwamko huu ni jambo la kupendeza na kufurahisha na unastahiki kuungwa na dua, ila kuna haja ya kutathminiwa kisha kukosolewa, kurekebishwa na kuongozwa.

### Sababu za Mwamko

Mwamko huu ni chimbuko la sababu mbali mbali, na mkusanyiko wa juhudi za vikundi na watu binafsi zilizopangwa na zisizokuwa na mpangilio wowote. Juhudi hizi zilikuwa za kiserikali kwa mara na za wananchi kwa mara nyengine. Tukio hili kwa asili ni ishara ya *fitra*, lathibitisha tamaa ya Umma wa Kiislamu kurejea katika uongozi na hali yake ya mwanzo. Pia ni dalili wazi kuwa dini hii ni dini iliyohifadhiwa na Allah *subhaanahu wa ta'ala.*

Anayezingatia Mwamko huu nakuazimia kuandika tarehe yake atakuwa na kibarua kigumu kuashiria mwanzo wake kwa wakati maalumu. Hii ni kwa sababu Mwamko huu na mfano wake una mizizi iliyokita kuanzia mbali, mizizi iliyodhihiri mara na kujificha mara nyingine. Pia ni juhudi zilizotanda, za wazi na zisizokuwa wazi. Kama vile, kazi ya da'wa au kulingania ni kazi yakuendelea na haitasimama; kazi ya kulingania hupata nguvu na

kudhoofika, na kupata mara na kukosea mara nyingine, lakini kuendelea kwake ni Sunna ya Ulimwengu na Sunna za Allah *subhaanahu wa ta'la* hazipotei wala kubadilika.

## Kushindwa mwaka 1967

Mwaka wa 1967 ulikuwa ni kipindi muhimu katika tarehe ya Mwamko wa Waislamu, kwani kushindwa kwa Waarabu dhidi ya Waisraili ilikuwa ni pigo kubwa na unyonge wa kina uliowafika watu kimawazo, kisiasa, kijamii, na kijeshi. Pigo hili-miongoni mwa athari zake-liliwachukiza viongozi mbele ya macho ya watu kwa kuwatia katika unyonge, pia watu wakaichukia na kuiacha misingi waliokuwa nayo hao viongozi kama vile fikra ya mageuzi ya kisiasa, kubuni jamii bila ya kutegemea mwongozo au misingi ya dini, ukomunisti, ujamaa, utaifa na *baathia* wakaanza kutafuta misingi na miondoko badala. Natija ya safari ya kutafuta ilikuwa ni kujisalimisha kwa misingi ya Uislamu. Uamuzi huu wakuukubali Uislamu si jambo la kushangaza kwani watu hawa walizaliwa Waislamu na walibakia Waislamu kisha jamii na watu binafsi hurudi kwa Mola wao wakati wa misukosuko na mitihani.

Kutokana na haya tunaweza kusema; kushindwa mwaka 1967 kuliupa Mwamko wa Waislamu msukumo mkubwa. Kwa hivyo tukio hili ni tukio kubwa katika tarehe ya Mwamko, na hekima ya Allah aliyetukuka inayojaalia kupatikana heri katika tukio la shari na shari katika tukio la heri. Hekima ya Allah inadhihiri pia kutokana na kanuni ya *Tadaafu'*, yaani; kanuni ya kushindana, kanuni daima na ya milele. Kila nguvu katika ardhi-ipende isipende-iko katika ushindani wakuendelea. Mara inashinda na mara nyingine inashindwa; katika mvutano huu kunapatikana fursa kwa wema na waovu, Waislamu na wasiokuwa Waislamu ili watende mema au uovu katika hali ya kuamiliana na mvutano huu, baadhi ya wema au waovu wakaamiliana na mvutano huu kwa uzembe au unyonge na wengine kwa nishati.

## Kanuni ya Mvutano

Uzuri wa huruma, rehema na uadilifu wa Allah aliyetukuka nikuweka kanuni kamili. Miongoni mwa kanuni hizi ni Kanuni ya Mvutano. Kanuni za Allah hazibagui mtu au jamii au dini. Watu wote mbele ya kanuni hizi ni sawa. Atakayefanya bidii kuzitumia kanuni hizi atafaulu awe atakaye kuwa, na atakaye zidharau atakhasirika awe atakaye kuwa. Miongoni mwa faida za Kanuni hii ya Mvutano ni kuwapa walinganizi matumaini kwa kubuni fursa, kuyahifadhi maisha kutokana na dhiki na unyonge, au kuendelea kwa hali isiyoridhisha na kuondoa ugonjwa wa ukinaifu. Kanuni hii pia huwakumbusha Waislamu daima kuwa anayemiliki dunia ni Allah aliyetukuka. Jambo hili huwazidishia Waislamu imani, utulivu, *tawakul* (kumtegemea Allah), utendakazi na kuimarisha nyoyo zao. Asema Allah aliyetukuka:

وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّفَسَدَتِ الْأَرْضُ وَلَـٰكِنَّ اللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى الْعَالَمِينَ

> Na lau kuwa Mwenyezi Mungu hawapambanishi watu kwa watu basi dunia ingeli haribika. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila juu ya walimwengu wote"
> [Al-baqara; 251].

Anayezingatia matukio ya mwaka 1967 anashuhudia kuwa Umma ulijitahidi kukabiliana na kushindwa huku na ukafaulu kwa jitihada kubwa. Miongoni mwa jitihada dhahiri ilikuwa vita dhidi ya Waisraeli mwaka wa 1973 na kuliangusha jeshi la mkoloni Sovieti, nchini Afghanistani mwaka wa 1989.

## Kuanguka kwa Umoja wa Sovieti

Mwamko wa Waislamu uliendelea kutanda katika dunia yote. Kuenea huku kulikabiliwa na makosa yaliyotofautiana baina ya nyakati mbalimbali na nchi mbalimbali kama vile masomo yaliyopatikana yalitofautiana baina ya sehemu moja na nyengine. Ingawa makosa yalipatikana, hayakuwa makosa yakubatilisha wema na usawa uliokuwa katika mwamko huu. Pia kadiri ya makosa hayo hayakuzuia gurudumu la mwamko kusonga mbele hadi kukapatikana tetemeko kubwa; nalo lilikuwa kuanguka kwa umoja wa nchi za Sovieti mwaka wa 1991 na kutawanyika kwake. Umoja huu uliokuwa mkubwa ulivunjwa kwa mikono ya wanawe wenyewe hadi kuwa nchi mbalimbali baada ya kuwa nchi kubwa iliyokusanya mataifa tofauti. Kuanguka huku kulisuhubiana na kuanguka kwa fikra ya kikomunisti (kupinga Uungu wa yeyote) iliyokubalika na umoja wa Sovieti; fikra iliyokuwa dhidi ya dini zote kwa jumla na Uislamu hasa. Kwa kuporomoka huku, dunia ilipata uhuru kutokana na dhalimu ambaye alingadamiza Uislamu na Waislamu. Kulipatikana fursa ya utendakazi na ulinganizi wa Kiislamu mkubwa na kuimarika katikati ya ardhi ya umoja huu ulioporomoka na kupatikana ufunguzi wa sehemu mpya za da'wah. Tetemeko hili ni natija na matunda ya Kanuni ya Mvutano na uwezo ni wa Allah mwanzo na mwisho.

## Minara miwili ya New York 9/11

Baada ya miaka kumi tangu kuanguka kwa umoja wa Sovieti tetemeko la tatu lilitokea nalo ni kupigwa bomu kwa minara miwili ya biashara mjini New York mwaka wa 2001. Baada ya tukio hili kulipatikana maelezo na tafsiri nyingi tofauti kuhusu wahusika, na huenda tukio hili litabakia ni kitendawili miongoni mwa vitendawili vya historia. Lakini tukio hili limefuatiliwa na uvamizi wa nchi ya Amerika kwa nchi ya Iraq na Afghanistan na kupatikana kwa madai mengi dhidi ya Uislamu na Waislamu katika vyombo vya habari, kisiasa, kiuchumi, kijeshi na kitamaduni. Mazungumzo haya yamewashugulisha wengi na kuwa hadithi za marafiki na maadui ulimwenguni kwa jumla na Uropa na Amerika hasa. Wengi wanaozungumza juu ya Uislamu na Waislamu ima wanazungumza kwa nia mbaya au kwa ujinga, wachache ndio wanaozungumza kwa uadilifu. Mazungumzo haya pamoja na shari na heri inayosuhubiana nayo, yamejaalia dini ya Uislamu kuwa na umuhimu kwa wengi. Jambo hili ni fursa nzuri; yafaa walinganizi katika uwanja wa da'wa kuwasilisha Uislamu kwa njia nzuri. Fursa hii pia ni matunda ya Kanuni ya Mvutano, na amri ni ya Allah mwanzo na mwisho.

Kana kwamba Allah aliyetukuka – na hekima ni Yake yote, anataka kwa matukio yaliyopita na yajayo kuilima ardhi yote kwa jumla. Matayarisho haya yataufanya Ulimwengu kuipokea dini Yake (Uislamu) iliyonyooka na walimwengu wakombolewe kutokana na upotofu na kuingia katika uongofu, na wakombolewe kutokana na dhiki na kupata faraja na raha.

### Maelezo Muhimu yanayohitajika

Liwe liwalo, yafaa Umma kufahamu kwa uzuri yafuatayo;

- Fursa hii adimu yakuueneza Uislamu itapita ikiwa walinganizi wenye ikhlasi na uhodari hawatoitumia vyema
- Sunna za Allah aliyetukuka hazitowatunuka Waislamu ushindi bure kwa kuwa ni Waislamu tu
- Yafaa wajitokeze baadhi ya vijana katika Umma wa Kiislamu walio na uhodari na wenye nafasi ili wasome na kuzingatia makosa yanayopatikana katika kazi ya ulinganizi kabla ya kujitokeza na kuwatahadharisha Waislamu na kurekebisha makosa baada ya kutokea kwa hasara chache iwezekanavyo

- Wafanye bidii kuzindua mipaka mipya na kutumia mbinu na ala tofauti za da'wa ili da'wah isigande na kupatikane kushindwa na unyonge
- Wazingatie kuimarisha kazi ya da'wa na kuikosoa
- Wafanye bidii kuleta uwiano baina ya walinganizi na kupunguza hitilafu baina yao.

## Matatizo na Matahadharisho

Hakika mwamko wa Kiislamu ulitanda kulingana na kadari, watu wakafurahia na kubashiri heri na wakaanza kubuni matarajio yao mema kwayo. Lakini ili ukamilike mwamko huu kuna umuhimu wa kusisitiza ya kuwa, kuna matatizo yameuzingira na kuutia dosari na kuzuia mwendo wake. Tunashuhudia da'wa ikitofautiana na da'wa nyingine, na mara nyingine kufanyiana uadui na kufanyiana vitimbi hadi kukatokea *fitna* na kuzidi uadui na farakano hadi wakadhania baadhi hitilafu hizi ziko juu ya Waislamu wote kwa jumla na walinganizi hasa kuwa ni jambo la hakika iliyo baini na ugonjwa wa kudumu na tatizo sugu; hajaokoka yeyote ila aliyenusuriwa na Mola.

Matatizo haya yanadhihiri zaidi pindi juhudi za wenye ikhlasi zinapokosea, na kujitahidi pasipo na haja au mara kuchagua yaliyo duni na kuwacha yaliyo bora na karibu, licha ya hayo ni kujitahidi katika yanayodhuru na kuudhi.

Pia walinganizi wengi katika uwanja wa da'wa ni watu wa kawaida na wanapenda heri, mambo mawili haya, hufikia daraja ya kughafilika. Ghafla hii huwapa fursa wenye shari kuwahadaa na kuwatia kwenye mitego ya kijinga na ya kuangamiza na kuwaudhi wao wenyewe na nchi na waja, kama vile kuwachukiza mbele ya macho ya waja na mara nyengine kuwafanya watu kuuchukia Uislamu, na kuuogopa. Huenda nyanja inayodhihirisha kutokufahamu kwao zaidi ni katika jukwaa la kisiasa. Juhudi nyingi na kujitolea kwingi kumepatikana, lakini wao ndio walikuwa wa mwanzo kukhasirika. Walilipa thamani ghali kama ilivyolipa nchi na wananchi thamani ya juu na hayo ndiyo ya hatari na aibu.

Hakuna shaka kwamba *dhahira* (dhihirisho) hii haiwezekani kuwa na sababu moja, lazima kuwe na sababu kadhaa mbalimbali ambazo zimeshirikiana. Baadhi ya sababu hizi ni sababu za ndani na nyengine za nje, miongoni mwa sababu hizi ni ujinga, kughafilika, kufanya haraka, kuiga kipofu, unyonge, kutokuzingatia Sunna za Allah aliyetukuka, matamanio ya nafsi yaliyovikwa vazi la dini na wanaotaka mali, uongozi na ukubwa. Pia miongoni mwa sababu ni kudura finyu ya kufahamu, na sababu zingine zatokana na hali ya zama au wakati unaoipitiwa na Umma. Wakati hatari wenye kutia dhiki na kuleta athari kubwa katika sehemu nyingi na miongoni mwa sehemu hizo ni da'wa ya Kiislamu.

Ikiwa uchambuzi huu ni sawa juu ya *dhahira* hii hatari, basi hakuna budi kukubaliana kuwa hakuna matibabu na suluhisho moja bali lazima kupatikane mkusanyiko wa mbinu mbalimbali za kusuluhisha.

## Mwanzo

Jambo la kwanza katika mkusanyiko huu wa mapendekezo na la umuhimu hasa ni kusahihisha misingi itakayotumika na walinganizi wote wa Kiislamu; hii ni kwa kuwa misingi hudhibiti – kwa jumla kiwango kikubwa – ubunifu wa fikra na mawazo ya mtu, na njia za kupima na kufikiria na sababu za kufanya jambo na kuwa na msimamo thabiti. Miongoni mwa mambo yanayokubaliwa na wote ni kuwa fahamu ikiwa makosa vitendo vitakuwa vya makosa na fahamu ya sawa itazaa vitendo sawa.

Mwanzo, hakuna anayedai kuwa kusahihisha misingi peke yake kutatatua *dhahira* hii, lakini hakika, kusahihisha huku katapunguza matatizo kwa kadiri kubwa.

Mwamko wa Kiislamu una haja ya kukosolewa, kurekebishwa, kusahihishwa na kurejelewa kwani vitendo vya mwanadamu hupata na kukosa. Ikiwa Mwamko huu unatishiwa kutoka nje bila shaka unatishiwa kutoka ndani pia, tishio la ndani lilikuwa tangu mwanzo na liko sasa na litabakia kuwa ndilo tishio kubwa na la hatari zaidi kuliko tishio la nje.

Ikiwa tishio la nje latokana na maadui mbalimbali wa Uislamu, basi tishio la ndani latokana na Mwamko wa Uislamu wenyewe; miongoni mwa tishio hili ni fahamu mbovu, au akili duni, au ubinafsi, au kufanya haraka iliyo kinyume na hali ya mambo au kutaka hali nzuri au mabadiliko yasiyowezekana na kadhalika.

Kutokana na haya kunapatikana haja ya Mkataba Adhimu uwasilishwe kwa walinganizi katika kazi yao ya da'wa. Mkataba utakaokusanya misingi asasi, ambayo, itawakusanya walinganizi wote au kukusanya idadi kubwa miongoni mwao. Mkataba huu wataraji kutoa mwongozo wa malengo pana yanayoshirikisha na kuwakusanya mahodari na wenye hima ya da'wa. Mwongozo unaokubali kwa kiwango fulani na kutofautiana ndani ya kiunzi kinachoshirikisha. Kwani watu hawawezi kuwa chapa moja inayoshabihiana katika kila jambo, jambo hili laweza kuitwa 'kutofautiana ndani ya kiunzi kimoja'.

Kwa sababu ya haya, na kuhisi masuulia na amana, na kutokana na msingi wa kupeana nasaha na kurekebisha makosa, nina furaha kutanguliza misingi hii asili ambayo naona kuyafahamu, na kunufaika nayo itapelekea mwamko wa Kiislamu kupiga hatua muhimu kwenda mbele ili uweze kutoa matunda yake yanayotarajiwa kwa heri kwa idhni ya Allah.

Yafaa kutajwa kuwa misingi hii ni natija ya juhudi, shida, mazingatio, marejeleo, masomo, kuangalia kwa muda mrefu makosa na usawa katika kazi ya da'wa. Kati yake, kuna misingi iliyotimu uandishi wake mwanzo nje ya uwanja wa da'wa, na mingine ilipatikana kwa tajriba ya dhiki au lafudhi ya baadhi ya misingi ilipatikana huku na kule ili kupatikane kuridhika nayo.

## Malengo ya Mkataba

Mkataba huu unakusudia kuweka mkusanyiko wa misingi ambayo yatarajiwa itakubaliwa na kuheshimiwa na wote. Yakitimu haya, basi kutapatikana mafanikio makubwa, miongoni mwa hayo ni; kupatikana kwa roho ya mahaba na kuaminiana baina ya walinganizi, kusikizana baina ya walinganizi wa kiserikali na wasiokuwa wa kiserikali, kupunguza sababu za hitilafu, kupunguza makosa na kuongeza sababu za kuelewana na kufaulu, kushajiisha kunasihiana kwa wema bila ya kuaibishana, na kufikiria kwa kina na kulenga mbali, kuvumbua mbinu na njia mpya, kusaidiana katika yanayokubalika na kusameheana katika yanayotenganisha na kujikomboa na hali ya kutokuwa na hila au uwezo na kufikia utendakazi.

Tukitaka kufupisha malengo ya mkataba huu kwa ibara fupi inayo ashiria madhumuni yake, tunaweza kusema unakusudia mkatabu huu, 'kuimarisha muelekeo wa da'wa, na kuleta uwiano baina ya walinganizi, na kulenga upeo mpya katika da'wa' kisha mkataba huu unawakusudia watu wote lakini kwa daraja ya kwanza na kimantiki unawalenga walinganizi kwani wao ndio wenye kufaidika nao, na wao ndio wenye uwezo wa kuurekebisha na kuongeza maoni yao.

Mkataba huu unakusudiwa kuwa ni nyaraka za kazi uliotokana na muelekeo wa Qur'ani Tukufu na Sunna sahihi mbali na kuacha maamrisho au kuvuka mipaka, yaani iliyokuwa kati na kati na iliyo adilifu. Nyaraka zisizo beba nembo ya kikundi fulani, au mkusanyiko hasa, au jamaa moja, au chuo cha da'wa, au jitihada ya *kifikihi*, au msimamo wa nchi fulani, wala haushinikizi sehemu fulani kinyume cha nyengine.

Vile vile Mkataba huu unalenga kuwa ni mfumo wa fikra, tabia, malezi, na utendakazi wa walinganizi na *hilfu fudhul* (mkataba aliyoushuhudia Mtume Muhammad (sallalahu alaihi wa sallam) utakaotegemewa na kukubalika na mchango wa da'wa usiokuwa wa kuigaiga, mkataba utakaochukua nafasi yake miongoni mwa michango ya da'wa mfano wake.

### Mkataba huu unakusudia hasa:

- dini ya Uislamu ambayo ndiyo njia ya uongofu wetu duniani na akhera
- Umma wa Kiislamu ambao ndio mama yetu, na tunajifakhiri na kujigamba nao
- kazi ya da'wa ambayo ndiyo shughuli muhimu maishani, nayo ni shughuli ya mitume na manabii
- nchi ambayo inaihami dini ya Uislamu, lugha yetu, urathi wetu, waja wa Allah, tarehe yetu, ulimwengu wa sasa na ujao
- walinganizi wa siku za usoni ili da'wa yao ifaulu zaidi kwa makosa machache.

Kwa madhumuni haya, Mkataba huu unanuia kuwa na sifa ya usawa, ukamilifu wa maudhui yake, uadilifu, usio bagua, uwazi, na njia ya kielimu isiyokuwa ngumu, na uandishi wa hali ya juu, na maneno mazuri. Anayeusoma Mkataba huu ahisi kuwa nyuma yake – kuna uhakika sio ndoto – kuna uhai ulio na upeo wa mbali unaotamaniwa, na upana na matarajio ya kweli kuihudumia kazi ya da'wa.

Yatarajiwa Mkataba huu utakuwa ni nuru inayoongoza na chanzo cha mapatano baina ya walinganizi na ushirikiano kwa hiari ya nyoyo zao na ikhlasi. Kutokana na lengo hili ndio limepatikana jina 'Mkataba Adhimu wa Kulingania' kwani umoja katika Mkataba huu unapatikana mwisho baada ya kujitolea na kujiunga kwa hiari na kwa nia halisi na uaminifu wa kina na kufurahia yaliyomo katika Mkataba huu.

Pia yatarajiwa kuwa Mkataba huu utarejelewa kwa undani na walinganizi hodari walio na ghera ya dini, kwa lengo la kufaidika na yaliyomo ya sawa na kubainisha makosa yake. Na kuongeza misingi mingine hadi kila chapa mpya ya Mkataba huu iwe bora kuliko iliyotangulia.

Mola wetu, tuafikishe kwa yanayo kuridhisha, na ututumie katika heri, na uturuzuku ikhlasi na kuiambata Sunna. Sifa zote za ukamilifu ni zako, twakusifu na kukutukuza hadi uridhie, na utukufu ni wako ukiridhia na baada ya kuridhia.

Swala na salamu zimshukie bwana wetu Muhammad na ali na sahaba zake.

**Hisham Al Talib**

**1430H/2009**

## MISINGI YA MKATABA

### 1. *Tauhidi* kamili

Tunamuamini Allah aliye na nguvu na kutukuka kuwa ndiye muumba wa ulimwengu na mwenye uwezo. Naye ndiye anayeabudiwa kwa haki na kusifika kwa sifa za uweza, ukamilifu na wema, Allah asiyekuwa na sifa yoyote ya upungufu, twampenda, twampwekesha, twamtukuza, twamuogopa, twamtarajia. Tunawalingania Waislamu wote kwa jumla na walinganizi hasa kuipa mada ya akida, fahamu, imani, hisia na tabia kipao mbele juu ya mada nyingine zote. Akida ndiyo asili na mwanzo muhimu kuliko mengine katika dini, akida ndiyo shina na matawi (*asl* na *furu'*), akida pia ni msingi unaosuhubiana na misingi mingine ya dini mwanzo mpaka mwisho; vilevile akida huambatana na maisha ya Mwislamu katika mambo yake yote. Akida si mlango katika kitabu atausoma Mwislamu kisha ageuza kurasa kuingia katika mlango mwingine; akida ni mlango wa mwanzo anaousoma Mwislamu na kubakia nao daima akiwa anaisoma milango mingine. Hakika, akida ni hali yakuendelea ya kimawazo, hisia na utekelezaji unaobaki na Mwislamu maishani na kumwelekeza katika uhai wake wote hadi mauti. Jambo hili lahimiza – miongoni mwa yanayohimizwa – kufahamu Mwislamu fahamu pana na ya kina mambo yanayolazimika kutokana na akida hii. Muhimu zaidi kati ya hayo ni: kumpwekesha Allah aliye na nguvu na aliyetukuka, kumpwekesha katika ibada na kutekeleza amri na hukumu zake. Vile vile ni wajibu kuelewa yanayoivunja na kuibatilisha akida na yanayomtoa mtu katika Uislamu kamili au baadhi yake. Miongoni mwa mambo yakustaajabisha ni kuwaona watoto wakiislamu wakihifadhi yanayovunja udhu bila ya kuhifadhi yanayovunja akida, haya yote yanahitajika japo kuna tofauti kubwa baina ya udhu na akida.

Tahadhari kuipuuza *tauhidi* na kuipunguza kuwa nguzo ya kuhifadhiwa; maandishi makavu wanadhania waliohifadhi kuwa wao peke yao ndio walioongoka na kuenea kati yao ghururi au kuhadaika na hisia kuwa wao ni bora kuliko wenziwao. Wakaamiliana na wenzao kwa tabia nzito na kiburi. Hakika imani yao ya kuwa wamo katika haki ni jambo la kusifiwa na la kutakikana, lakini yafaa imani hii iambatane na upole na kuamiliana kwa wema na watu wengine. Kwa sifa hii nzuri, watakuwa ni walinganizi wenye kupendeza na kupendwa, sio wenye kuchukiza, walinganizi wenye huruma sio wakali. Ikiwa *tauhidi*i itakuwa hivi natija yake itabuni uzuri wa fikra, dhamira na tabia.

### 2. Uislamu dini ya Allah

Twaamini kuwa dini ya Uislamu ni dini ya Allah aliye na nguvu na utukufu, dini ya milele yenye kuhifadhiwa, dini iliyo sahihi na ya mwisho. Dini hii kwetu ni jambo la kutumikiwa, kitambulisho chetu, suluhu ya yote. Uislamu ni mwanzo wetu, maisha yetu ya sasa na yajayo. Dini hii ndiyo njia yetu ya kuongoka na mafanikio yetu duniani na akhera, ndiyo mfumo wetu aliyotuchagulia Allah aliye juu; twaiamini, twajifakhiri nayo, twajitolea kwa hali na mali kwa ajili yake na kuikomboa kwa kila kilicho ghali na azizi kwetu.

### 3. Kurudi katika misingi yetu ya dini (Qur'ani na Hadithi)

Kwa sababu sisi Waislamu twawapendelea watu wote heri, na kwa sababu sisi tumekalifishwa kuwalingania juu ya Uislamu, twawalingania waujue Uislamu kupitia asili yake kwa nyoyo kunjufu na akili ya uadilifu isiyolemea upande wowote kwa

imani kuwa wataongoka kuiona nuru baada ya kuishi katika giza, na kuipata haki baada ya upotofu na watapata ndani ya Uislamu suluhisho ya matatizo yao yote na jawabu la kila suala.

**4. Ilani ya mwanzo kuhusu haki za kibinadamu**

Twaamini kuwa dini ya Uislamu ndiyo ilani na mwito wa kwanza wakutetea haki za binadamu. Uislamu ni dini inayompa kila mwanadamu haki zake kamili; uhuru wa kidini, heshima na kadhalika mbali na haki ya kuelimika, kuoa au kuolewa, amani, uhuru wa kutafuta riziki, usawa, haki ya kumiliki, na haki nyinginezo. Uislamu unakusudia kumtukuza mwanadamu kwani yeye ni mbora wa viumbe vya Allah aliye na nguvu aliyetukuka; mwanadamu ndiye khalifa wa Allah katika ardhi na kila kilichomo katika ardhi kimeumbwa kutumiwa na mwanadamu.

**5. Wanadamu ni familia moja**

Twaamini wanadamu wote ni familia moja, undugu wa kibinadamu watujumuisha sote na muumba wetu ni Allah aliye juu. Baba yetu sote ni Adamu na mama yetu ni Hawa. Tumeumbwa kutokana na mchanga na mchangani tutarudi. Kutokana na haya twawalingania wote Waislamu na wasiokuwa Waislamu kushirikiana katika mambo yanayotunufaisha sote. Miongoni mwa haya ni: kuhakikisha kupatikana kwa amani, uhuru, kusimamisha uadilifu na kupigana na uhalifu, kueneza elimu, malezi bora, kuwatunza wazee, ujirani mwema, kuhifadhi mazingira na kuheshimu na kulinda mikataba na ahadi.

**6. Kulinda ndoa**

Ndoa ni makubaliano baina ya mume na mke, nayo ndiyo njia ya ki pekee inayotambulika kisheria kujenga familia. Ndoa hii ndiyo asili ya malezi na yafaa kupewa umuhimu zaidi. Familia ndiyo msingi adhimu wa jamii na chanzo asili cha kupata na kuwalea watoto. Idara ya familia ni jukumu la baba na mama pamoja, kwa hivyo kuna umuhimu wa kuhifadhi, kulinda na kuipa ndoa na familia umuhimu unaofaa. Yafaa pia kubuni njia na mbinu za kuifanya ndoa na familia kufaulu, kama vile yahitaji kusimama wima dhidi ya hoja, mbinu na majaribio yoyote yakuiharibu au kuivunja ndoa na familia kwa njia moja au nyingine.

**7. Kupokea mamlaka kwa njia ya salama na amani**

Ni wajibu wa walinganizi kujitahidi kufikia njia za busara na uwazi watakazo jilazimisha nazo. Mbinu hizi zitawahakikishia kupokea mamlaka ya taasisi za da'wa kwa amani, mapenzi na maridhiano. Msingi huu utapunguza ubinafsi na kupokeza kiongozi uongozi wandani wake, pia utapunguza fitina, kukatana na kuondoa hali ya kushindwa na kuganda katika hali moja. Utatoa fursa na nafasi kwa watu kuendelea na kuleta natija mpya. Utadumisha kupatikana kwa mawasiliano baina ya vijana na wazee na kufunza idadi kubwa ya vijana juu ya uongozi na kueneza hisia za umoja katika kazi na kuheshimu kazi ya taasisi kinyume na ubinafsi au kazi ya mtu mmoja bila ushirikiano.

**8. Msingi wa nuru**

Twapenda heri, undugu na kusaidiana na watu wote. Twawapa udhuru hata tunaotofautiana nao kulingana na msingi wa nuru wa shekhe Muhammad Rashid Ridha aliye mashuhuri – Allah amrehemu – asema; "Tusaidiane katika yale tunayokubaliana na tusameheana katika yale tunayotofautiana".

### 9. Shura

Twalingania msingi wa kushauriana na kuhimiza uhodari wa fikra na uvumbuzi na kuheshimu rai zote ziwe tofauti au zinakubaliana na rai zetu. Twampa kila mtu haki ya kujieleza na kutoa maoni yake. Msingi huu utafaulu ikiwa watu wote watajilazimisha na rai iliyoafikiwa maadamu haiendi kinyume na misingi ya sheria iliyokubalika na iliyo wazi. Ili msingi huu uwe wa sawa au karibu na haki, lazima upatikane kutoka kwa taasisi zinazokubalika pekee. Kwa hivyo, inabidi kiwango cha elimu na maelezo msingi kuwa kamili kama vile vile inatakikana juhudi za kweli zenye lengo mahususi na uaminifu kutumika.

### 10. Uongozi

Da'wa yafaa kutahadhari sana na vitovu viwili vya uongozi, kimoja rasmi na dhahiri lakini kisichokuwa na athari mfano wa picha; na cha pili cha siri kilicho na uwezo wa kufanya kitakacho na kina athari ya kushuhudiwa. Cha kwanza kina umaarufu (picha dhahiri) na cha pili kina vitendo. Kitovu cha siri ndicho kilicho na uwezo wa uamuzi pekee, kinaathiri kitovu rasmi na kina ushawishi mkubwa wa kugeuza mambo yaende kulingana na matakwa yake au kukifanya kitovu rasmi kulazimika kufuata rai yake. Hakika jambo hili ni ukosefu wa uadilifu na ni kinyume na misingi ya kazi ya da'wa inayotakikana kuwa ya kushauriana hasa msingi wa shura. Pia vile vile msingi wa kazi ya pamoja unaepusha kukubaliana katika mambo yaliyo kinyume na sheria. Uongozi aina huu ni uongozi wa mabavu ulio wazi na uongozi wa mabavu katika mambo ya kidini ni ovu kuliko mambo ya kidunia. Hii ni kwa sababu uongozi kama huu huvishwa vazi la dini kwa malengo ya wanaohusika. Kawaida ya hali hii ni kitovu cha uongozi wa siri huwa na dharau na kiburi juu ya kitovu cha uongozi dhahiri. Nacho kitovu cha uongozi dhahiri hukichukia kitovu cha uongozi wa siri na kutamani kuangamia kwake kama vile kudhoofika na kuwa kejeli. Haya yote huchangia kupatikana uadui, chuki na kuleta kushindwa na unyonge. Hakika kuwa na vitovu vingi vya uongozi vinapodhihiri vinaangusha da'wa na vimesababisha thamani chungu kwa da'wa.

### 11. Kuinadhimu kazi ya ulinganizi

Twaamini kazi ikiwa rasmi ya pamoja yenye nidhamu, na inaheshimu tabia za Kiislamu, nakuchunga nidhamu na sera za kazi, ina manufaa zaidi kwa Umma wetu. Kazi ya sampuli hii inadumu zaidi kuliko kazi ya mtu mahususi au inayotegemea mtu mmoja. Ingawa katika kazi zote mbili yapatikana heri, bila shaka kazi ya pamoja inaweza kupimwa kwa njia rahisi, kusahihishwa, kurekebishwa, na kuvumbua mapya. Kisha watu binafsi huondoka na kufa ama kazi ya taasisi hubakia na kuendelea.

### 12. Roho ya ushirikiano kazini

Tunahimiza kuimarisha roho ya ushirikiano baina ya walinganizi, na kubuni fahamu ya kina ya msingi wa ushirikiano baina yao. Miongoni mwa juhudi za kuimarisha ushirikiano ni kuwaheshimu waliotangulia katika kazi ya ulinganizi na kushajiisha mawasiliano baina ya rika mbalimbali ili tufaidike na hekima ya wenye umri mkubwa katika kazi ya ulinganizi na hamasa ya vijana. Kutanguliza maslahi ya wengi juu ya maslahi ya wachache au mmoja na kukubaliana njia za kisheria zitakazotumika kuzuia matatizo na hitilafu kabla ya kuzuka. Kusuluhisha matatizo na hitilafu baada ya kutokea kwa mbinu bora, na kueneza roho ya uadilifu katika matumizi na idara.

**13. Kuwalea wenye vipaji**

Twaamini kuwa wanafunzi wenye vipaji wafaa kushughulikiwa kwani wao ndio viongozi wa maendeleo na mabadiliko, wenye kutoa suluhisho badala zenye faida na juhudi katika siku za usoni.

**14. Mfano wa kuigwa**

Yafaa kila taasisi ya da'wa iwe na misingi, mfumo, na mipango na tabia za wafanyikazi wake hasa ambazo ni mfano mzuri wa kazi ya ulinganizi wenye hekima ambao wakiuona wengine wanaustaajabia na kuuchukua kama mfano wa kuigwa.

**15. Mabadiliko yanayolenga mbali**

Twaamini umuhimu wa kupatikana mabadiliko na utohozi wakuendelea bila ya kuivunja misingi thabiti ya dini. Kwa kubadilika huku tunaweza kujumuisha baina ya mema ya zamani na manufaa ya wakati tunaoishi kama vile kunapatikana utohozi na wakati tunaoishi na kuyaelewa mambo ya kileo. Kufanya hivi kunatupa sisi uhai ambao unatukinga sisi na kuganda kwa yanayotudhuru na kututia unyonge na kujitenga na ulimwengu kinyume na maamrisho ya dini yetu.

**16. Kujitegemea**

Twalingania na kuhimiza kupatikane kujitegemea kikweli na kutosheka na uwezo wetu kadiri inavyowezekana. Misaada si tegemeo, hakika yake nikuwa hukatika na haidumu. Huenda tegemeo badala na zuri ni kujenga wakfu zinazoambatana na uwezo na hali za wahusika.

**17. Sheria zisizobagua**

Hakika Sunna ya Mwenyezi Mungu aliye na nguvu na uwezo – kwa uadilifu na rehema Yake kwa waja – ni sheria zisizobagua na ni sheria za kudumu, hazipendelei yeyote wala kumchukia yeyote, watu wote ni sawa mbele ya sheria hizi. Yeyote atakayeamiliana na sheria hizi atafaulu kwa yake, awe atakayekuwa na atakaye ziasi ataporomoka awe atakaye kuwa. Maana ya haya ni kuwa, Allah aliye na nguvu na uwezo, hamtunuku yeyote au kikundi chochote miongoni mwa vikundi vya Waislamu ushindi wa bure kwa kuwa ni Waislamu bila ya kujitahidi na kutumia sababu za kufaulu.

**18. Haja ya kujipumbaza**

Kujipumbaza au vinavyoleta furaha-bila ya kupita mipaka- ni miongoni mwa mambo muhimu yanayoimarisha uhusiano baina ya wanaolelewa na jamii zao. Kujipumbaza huku kunabuni ghera na kuwaunganisha watu na kuwafanya kuaminiana na kukubaliana na maadili ya na fikra za jamii yao. Kwa sababu ya manufaa haya tunahimiza jambo hili kusisitizwa katika kila fursa na nyakati mbalimbali kama vile sherehe za Idi, sherehe za mwanzo na mwisho wa mwaka wa masomo. Yafaa kusimamisha sherehe, mashindano, michezo tofauti na kuimba kasida na kuzawadiwa washindi na mengineo ya kuwapumbaza na kuwafurahisha wanafunzi.

**19. Malengo na mbinu**

Misingi ya asili ni thabiti na haibadiliki, ama njia za kuyafikia malengo thabiti huambatana na wakati. Kwahivyo yafaa njia hizi na mbinu zinazotumika kubadilika kulingana na wakati na yapasa pia zitohozi tajriba ya waliofaulu Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Kwani hekima ni lengo la Muumini, kisha kila njia miongoni mwa njia za kazi ya ulinganizi yategemea misingi miwili; kwanza, kuweko kwa haja ya kweli yakuianzisha kazi ile, na pili matunda yanayopatikana yawe mengi kuliko madhara; ikiwa kinyume cha haya, kazi ile isifanyike.

**20. Uislamu na kazi ya Uislamu**

Uislamu ni dini na kazi ya kulingania ni mambo mawili tofauti lazima yatofautishwe. Uislamu ni dini ya Allah iliyosahihi na itakayobakia milele na haikuwa na dosari au upungufu na wala haitapatikana na dosari wala upungufu. Ama kazi ya ulinganizi ni juhudi za wanadamu hupata na hukosea, lakini dini ya Allah aliye na nguvu na uwezo imehifadhiwa na makosa. Vitendo vya kuineza dini havijahifadhiwa na makosa na utukufu wa dini ya Uislamu hauivuki na kuufanya kubakia bila ya utukufu wake.

**21. Utaratibu (*manhaj*) ulio bora**

Nidhamu iliyo bora kutumika kuwalingania waja ni kuwafahamisha misingi ya Uislamu na nidhamu zake kwa usawa, uwazi na ukamilifu. Kufanya hivi kutamsaidia mja kufahamu na kuelewa dini kwa urahisi. Pia ni haraka kukubaliana na Uislamu. Na tutahadhari kuwasilisha Uislamu kwa kueneza shaka au masuala yaliyo na utata na kuwadhiki waja kwa hoja tofauti. Haifai pia kuwaanzisha watu kwa masuala ya vikundi mbalimbali vya Kiislamu, fikra na jitihada na maoni waliyonayo hawa kinyume na wale, na uzuri wa hawa juu ya wale na kinyume chake. Kukipatikana haja ya kuyaeleza masuala kama haya basi yafaa kujibiwa kwa kifupi bila ya kuivunja misingi ya dini.

**22. La kwa midahalo**

Msingi huu unahimiza kuufunga mlango wa midahalo ya kinadharia au kueneza misimamo na rai zilizokwenda kinyume na rai na misimamo ya *jamhuri* (wengi) ya wanachuoni au jitihadi iliyokataliwa au kujadili mambo hayatarajiwi kutokea na mijadala isiyo na maana. Kujishughulisha na haya ni kupoteza wakati, juhudi na mali. Mbali na ya haya, mijadala hii huwashughulisha watu na kuwatoa katika majukumu msingi ambayo yafaa kuangaliwa na pia – aghlabu ya wakati – huleta na kuongeza chuki, kutofautiana hata kufikia hali ya kubebeana kisasi na uadui.

**23. Uhusiano mwema baina ya taasisi za da’wa**

Asili ya kuamiliana baina ya vyama vya Kiislamu ni kukamilishana, ikishindikana yafaa kushirikiana na likiwa zito pia hili basi waheshimiane na kuvumuliana ama wakichagua jingine basi ni maangamio.

**24. Umuhimu wa tathmini**

Hakika msingi wa kutathmini ni msingi wa Kiislamu tangu jadi, na ni njia ya kisasa yenye kuheshimiwa. Yatupasa sisi kuuchunga msingi huu na kutathmini mambo yetu kila mara kwa kuelezana ukweli, kufichua makosa, kujirudi mtu binafsi, kukagua kila wakati, na kuangalia mafanikio, matatizo na makosa ili tutambue nukta nzuri tuzihifadhi na kuziongeza na kutambua makosa tuyaondoe na kuepukana nayo kwani kazi ya mwanadamu hupata na hukosa.

**25. Kuheshimu wataalamu**

Msingi huu wahimiza kuwauliza na kutaka msaada wa wasomi wa dini kuhusu masuala ya dini, na tuwaulize wataalamu na wenye weledi fulani masuala waliyo na ujuzi nayo. Huenda fulani miongoni mwa watu ni mlinganizi mashuhuri aliye afikiwa lakini hafai kufutu kwa ukosefu wa elimu msingi na wala hana taaluma mahususi.

**26. Roho ya kujenga**

Roho ya kujenga yahimiza na kusisitiza kuwa na mawazo na fikira nzuri za kujenga, kutarajia na kutumaini mambo yatatengenea, kutoa bishara njema, na kuwafanyia watu wepesi. Haifai kuwafisha watu moyo au kuwafanya wasiwe na mategemeo ya baadaye, yaso rajua, kuwachukiza watu na kuwafanyia ugumu katika dini.

**27. Haja ya makini**

Kuna haja ya kutumia hekima na umakinifu katika shughuli zetu zote na kuacha kufanya mambo bila ya kuzingatia matokeo yake. Pia ni wajibu kuwa watulivu na kuwacha hasira zitawale fikra zetu na kuelekeza vitendo vyetu. Twahitaji kujihusisha na kuwa mahodari wa maisha na yanayojiri kinyume na hali ya kuzembea na kutupa majukumu.

**28. Dini kamili**

Uislamu ni dini ya mwisho ya Allah mwenye uwezo na nguvu. Kwa kuwa dini hii ni ya mwisho ina nidhamu kamili inayoongoza maisha kamili ya mwanadamu kuanzia mtu binafsi, familia, jamii, kikundi na nchi. Dini hii ina mwongozo kwa nchi, na kuongoza kanuni, ibada, mfumo wa mali, tabia, siha, uhusiano wa mtu na mke wake, jamii, uhusiano baina ya nchi moja na nyingine na kadhalika. Dini hii ina mwongozo kuanzia utotoni, maishani, mauti na kufufuliwa kwa waja. Kwa sababu ya ukamilifu wa dini ya Uislamu yafaa walinganizi kuhimiza msingi huu na kuonyesha fahari yake na kukanusha juhudi za kuudhihirisha Uislamu kama dini ya maamrisho na makatazo (ibada). Msingi huu unafundisha kutokushughulika na yasiyokuwa asili au ya msingi na kuyaacha ya msingi; kukiwa na dharura ya kuingilia na kufanya mojawapo ya jambo lisilokuwa la msingi basi yafaa kulifanya kwa kadiri ya dharura ile bila ya kuvuka mipaka.

**29. Adabu ya majadiliano**

Adabu ya mazungumzo na majadiliano na ujuzi wake ni jambo muhimu kwani mazungumzo ni miongoni mwa mbinu za ulinganizi zilizofaulu. Aliye hodari wa

kuzungumza na watu ni wakili wa anayolingania kwayo na kinyume cha sifa hii atakuwa akiitusi dini na kuichafua.

## 30. Nukta zinazojumuisha

Haiwezekani walinganizi wote kuwa na lengo moja au kutumia mbinu sampuli moja wala kuyapa uzito mambo kwa mfumo mmoja. Lazima kupatikane tofauti baina ya walinganizi iwe tofauti yenyewe kubwa au ndogo. Lakini akichunguza mtu jambo hili ataona kuwa kuna nukta na sifa nyingi wanazoshirikiana walinganizi wengi kama vile akida, ibada, tabia, na kuamiliana na watu kwa wema isipokuwa sifa hizi –kwa ushindani na uadui baina yao- hupotea. Kwani kugongana huonyesha tofauti nyingi na kuyafanya madogo kuwa makubwa na makubwa kuwa madogo. Ama ushirikiano hupunguza hitilafu na kudunisha tofauti baina ya watu. Kwa mujibu wa haya, twaweza kusema kwa hakika kuna mambo wanayokubaliana walinganizi na wanayoshirikiana. Ni jukumu lao wote wayajue mambo hayo, kuyafurahia na kuyatumia ili kuboresha ushirikiano baina yao bila ya kuharakisha matunda ya umoja huu wa sifa na mienendo kwa uvumilivu na kudumisha jitihada hizi ili kuwajumuisha walinganizi wengi iwezekanavyo.

## 31. Hatari ya usiri

Kuna hatari ya kuifasiri dini vibaya na kuunda vikundi vya siri vinavyoficha itikadi zao na vitendo vyao. Uislamu kama dini iliyo kamili ni dini iliyo wazi na misingi yake na fikra yake iko wazi. Hakuna siri wala usiri katika mambo ya dini na hakuna kuongeza chochote katika Uislamu. Kudhihirisha itikadi ya Uislamu ndiyo nguvu ya Uislamu, kawaida, mtu hujionyesha na kile anachofurahia kama vile watu wanaukubali Uislamu kutokana na kufahamu kwao fikra zilizo wazi, bayana na zenye kufahamika kupitia *fitra* aliyowaumba kwayo Mola. Kwa *fitra* hii pia, hujitenga na fikra za siri zisizofahamika zinazopotosha. Usiri huwadhuru wenyewe zaidi ya mahasimu wao kama vile usiri wa jambo hulifanya likatisha kwa sababu ya giza lake kutanda kinyume na makosa ya uwazi kwani makosa yanayofanyika mchana huonekana katika muangaza.

## 32. Umoja wa fikra

Miongoni mwa tofauti baina ya walinganizi wa Kiislamu ni kukosekana umoja msingi au aina yoyote ya kushirikiana kimawazo. Jambo hili limeathiri na laendelea kuleta tofauti baina ya walinganizi katika malengo yao ya da'wa, mbinu wanazotumia na fikra tofauti zinazowafanya kuona malengo na mambo fulani ni aula kuliko mengine licha ya kujenga chuki na kisasi. Kwa sababu hii, kuleta umoja wa fikra baina ya walinganizi kwa jumla na vijana hasa ni jambo lahitaji kupawa kipao mbele. Umoja huu utatimia kwa kufundisha elimu ya dini kwa misingi ya Qur'ani na Sunna, uadilifu, ushirikiano, kusameheana, undugu, ukweli, pamoja na fahamu ya nini kinachofaa kutangulizwa mbele ya vingine, na ujuzi wa kujadiliana na adabu za kutofautiana, na kuhimiza ukamilifu wa dini ya Uislamu na kipi kinafaa kwa kila wakati na kila sehemu.

Miongoni mwa vitu vinavyosaidia fahamu ya haya ni kuafikiwa kuvichagua vitabu vinavyooana na lengo hili na kuviweka karibu na walinganizi na vijana na kuvirudia vitabu hivi mara kwa mara kama vile vitabu vya shule hurudiwa mara kwa mara na wizara ya elimu ili kuhakikisha utohozi wake na matakwa ya wakati na sehemu.

### 33. Kuheshimu sio kutukuza

Ni kawaida na *fitra* kwa Mwislamu kumpenda kiongozi wake awe mwanachuoni au imamu wa msikiti wake. Jambo hili halipendezi tu bali lina manufaa. Mapenzi haya hayafai kupita mipaka; baadhi ya walio tutangulia katika dini nyingine waliangamia kwa kuwatukuzu manabii na wema wao na kuwaabudu dhidi ya Allah. Jambo hili liliwaingiza katika ushirikina baada ya kumpwekesha Allah. Miongoni mwa maradhi yanayowapata Waislamu wa kawaida na walinganizi ni mafungamano yao na marejeo yao ya kielimu na kidini, mafungamano yaliyopita mipaka. Wamewafanya mashekhe na vyuo vyao kuwa ndio kipimo cha kutofautisha baina ya haki na batili na sawa na makosa licha ya kuwa mashekhe na vyuo hivyo havijahifadhiwa na makosa. Wamesahau kaida isemayo; '*Twawajua watu* (wakweli) *kwa* (kuifuata) *haki, wala hatuijui haki* (kuwa ni haki kwa sababu ya fulani) *kwa watu*'.

Kuwatukuza watu kunaendelea kuwa pigo kwa Waislamu. Kumeleta hitilafu, chuki na ushindani baina ya walinganizi. Suluhisho la donda ndugu hili ni watu kupenda marejeo yao ya kielimu na da'wa kwa uadilifu na wawaone kuwa ni wanadamu hupata na hukosea. Wanaheshima, kupendwa na kufuatwa kwa kadiri ya haki waliyonayo. Kila Mwislamu anatafuta haki, wanachuoni na walinganizi ni njia yakuifikia haki, nao huondoka, na maoni -ndiyo lengo- hudumu na hubakia.

### 34. Kuendelea walipoacha wengine

Da'wa haianzi sasa, yafaa walinganizi kufaidika na tajriba za waliotangulia. Taasisi tofauti kama chuo na mlinganizi sio wa mwanzo kuihudumia dini hii ya Allah na wala hawatakuwa wa mwisho.

### 35. Sunna ya hatua kwa hatua

Kuelewa msingi huu kuna matunda mengi na msingi huu unalenga kufahamisha maana ya kutambaa kabla ya kutembea, kupanda kabla ya kuvuna, na kutumia hekima badala ya hasira. Unafundisha juhudi za kudumu sio juhudi za haraka zisizo dumu. Imepokelewa katika hadithi za Mtume (rehma na amani zimshukie yeye);

"*Amali iliyo bora na inayopendwa zaidi na Allah (sw) ni amali yenye kudumu hata ikiwa ndogo*" [Muslim].

*"Hakuna anaye ikokota hii dini ila humshinda"* [Bukhari].

Imepokewa na Jabir bin Abdullah, radhi ya Mola imfikie, *"Hakika aliyetangulia (na kuwaacha wenzake kwa kuharakisha kisha hakufikia lengo) hajaipasua ardhi wala hakubakisha kipandio chake kwa kukitumia vibaya hadi kikaharibika"* [Sharhu Sunna na Majmau Az-Zawāid].

Yahitaji tukumbuke methali isemayo “Wakati ni sehemu ya tiba”.

**36. Kwenda na wakati na hali**

Yafaa kugawanya malengo katika daraja tofauti ili malengo haya yahudumie lengo msingi kisha malengo daraja ya kwanza yatufikishe katika daraja ya pili na kuendelea kwa mfumo huo. Kama vile kuangalia malengo gani yawezekana kulingana na wakati na hali zinazozingira ulinganizi.

**37. Taasisi za uongozi wa pamoja**

Dini ya Uislamu ni dini iliyo hai na yafaa kila wakati na kila sehemu. Dini hii ina uwezo wa kusuluhisha matatizo mapya, na kwa sababu hii yafaa wanachuoni wa Kiislamu kutoa mwongozo wa matatizo yanayowakumba Waislamu siku hizi. Ni jambo zuri kupatikane taasisi zitakazofanya jitihada kwa pamoja mfano; wa taasisi hizi ni Chuo cha Utafiti wa Kiislamu cha Misri (*Majma' al buhuth al Islamiya fi misr*), Chuo cha *Fikihi* ya Uislamu katika Taasisi ya Umoja wa nchi za Kiislamu (*Majma' al fiqhi al Islami fi Rabita al Aalam al Islami*), Chuo cha *Fikihi* ya Kiislamu cha Khartum (*Majma' al Fiqhi al Islamiy fi Khartoum*), Kikao cha Uropa cha *Fatwa* na Utafiti (*Al Majlis al Urobi lil iftaa wal buhuth*), Kikao cha *Fikihi* ya Kiislamu Amerika Kaskazini (*Majlis al fiqhi al Islami fi Amrika ash Shamaaliya*), Umoja wa Wanachuoni wa Kiislamu Ulimwenguni (*Al itihaad Al aalamiy li ulamaa al Muslimiin*) na taasisi nyinginezo. Kuanzisha taasisi kama hizi kuna umuhimu na itakuwa jambo zuri kama taasisi hizi zote zaweza kushirikiana pamoja kwani kufanya hivi kutaleta faida kubwa. Pia ikiwa wanaohusika watakuwa ni watu wenye ujuzi na tajriba ya kazi zao, itazifanya taasisi hizi kuaminika na kuleta matokeo yanayotakikana.

**38. Kundi la Kiislamu**

Kundi lolote, jamii au harakati ya da'wa ni miongoni mwa jamii ya Waislamu lakini kundi au jamii fulani hawahesabiwi kuwa wao ndio Waislamu na wengine ni wafuasi wa kundi au jamii ile. Thamani ya kundi au jamii husika imo katika usawa wa kuifuata dini, fikra na natija ya kazi na utekelezaji wa haki.

**39. Hatari ya kujumuisha**

Ugonjwa ulioenea kwa walinganizi wengi ni kujumuisha na kutoa matamshi na hukumu za jumla. Mfano, kuhukumu kuwa dola kubwa zisizokuwa za Kiislamu hazikutani ila kuupiga Uislamu, na Mayahudi ndio wanaongoza ulimwengu wote kana kwamba wana uwezo wa kila jambo, na kila taasisi ya da'wa ya kiserikali ni mbinu ya kuwahadaa na kuwapotosha na yafaa kujihadhari nayo na kila juhudi za da'wa zisizokuwa za kiserikali ni nzuri na sawa na zafaa kuungwa. Mstari unaobainisha baina ya haki na batili ya mtu au kikundi ni kuimarika au kudhoofika kwake. Vile vile imani kuwa wasiokuwa sisi wana nia mbaya katika kila jambo walifanyalo na hayapatikani haya kwetu au kwa walionasi. Imani hii ina lemea upande mmoja na imekosa uadilifu na kuyachungua mambo juu juu bila ya makini.

Kuhukumu kwa haraka haraka bila ya kujishughulisha kuchunguza wala kusoma hali ya mambo na kutoa ufumbuzi na kujitahidi ni donda ndugu ya kazi ya da'wa. *Dhahira* hii imewafanya walinganizi kujiona hawana lawama kwa kuzembea na kutokuwa na mawazo ya kujenga. Walinganizi wengi – kama waonavyoona, au wanadhania wanaona, au wanaitakidi – kuwa mbele yao kuna adui mwenye uwezo mkubwa na shari baini, hawana uwezo wakukabiliana naye. Mawazo haya yanakwenda kinyume na Sunna ya Allah ya mvutano baina ya haki na batili.

Yafaa Mwislamu atahadhari na kujumuisha na kutoa hukumu za jumla zinazodhuru na mifano yake. Yampasa kuasha nuru ya akili yake na kuuhamasisha moyo wake na kujihami na ujuzi wakutatua matatizo na kuyaweka mambo mahala pake. Yahitaji kuunganisha baina ya tukio na sababu zake na baina ya natija na kiini chake na kujifundisha ujuzi wa kufumbua na ufumbuzi kinyume na hali ya kuzembea katika dhana na hisia kuwa hakuna hiari ima nyeusi au nyeupe, heri au shari, rahisi au lisilowezekana, unyonge au vita.

### 40. Wajibu wa wanadamu

Mwenyezi Mungu ameahidi kuihami na kuihifadhi dini hii ya Uislamu, lakini – kwa hekima Yake na hekima Yake ni kubwa - amewapa jukumu hili Waislamu. Ingawa Uislamu ni dini ya haki, inakwenda kulingana na kadari ya Allah kupitia juhudi za wanadamu. Juhudi na kujitolea kwa mitume na manabii (rehma na amani ziwafikie) pamoja na wafuasi wao ni jambo wazi kama vile waliokuja baada yao pia walijitolea mhanga kuipigania na kuihami dini hii. Waislamu wa leo lazima wawaige waliotangulia kama wanataka kuihifadhi dini hii kwa kuiga misingi na njia walizotumia.

### 41. Mfano mwema

Walinganizi na taasisi za da'wa zafaa kuzingatia kuwa mfano mwema ni miongoni mwa njia bora na yenye mafanikio katika kazi ya kulingania. Walinganizi waliotangulia walifaulu kueneza Uislamu kwa njia na mbinu tofauti; mbinu iliyotangulia mbinu zote ilikuwa ni kuwa mfano mwema na kielelezo chema. Kwa hivyo yawapasa kutanguliza mwanzo kabla ya lolote wawe wao ni mfano mwema kwa wengine katika yale wanayolingania kwayo.

### 42. Misamiati thabiti

Kuna haja ya kuwa waangalifu katika matamshi yetu. Yafaa tuwe na misamiati maalumu na thabiti iliyo wazi mbali na misamiati inayotumiwa na wasiokuwa Waislamu. Uchaguzi wa misamiati hii yafaa uwe wa makini na hekima. Haifai Waislamu kuingia katika mikondo ya kisiasa ambayo inapatikana muda baada ya muda. Uislamu haufai kutambulishwa kuwa ni ujamaa wakati falsafa iliyotanda ni falsafa ya ujamaa, au ubepari ikiwa muelekeo wa watu ni muelekeo wa ubepari, au demokrasia wakati Ulimwengu umeivaa fikra ya demokrasia na kadhalika. Uislamu ni Uislamu kwa misingi, fahamu na malengo yake, unakubaliana na kushirikiana na

baadhi ya misingi na mifumo ya kilimwengu kwa ukamilifu wake, lakini kufanana huku hakufai kuutambulisha Uislamu kwa mfumo huu au mwingine wa kilimwengu. Uislamu ndio asili, thabiti na haki ama mifumo hiyo ni fikra za wanadamu zenye kubadilika na kuachwa.

### 43. Uandishi

Uandishi wa da'wa unahitaji kuwa na mwelekeo mmoja, malengo yake yadhibitiwe ili kupatikane risala moja itakayofahamika na wasomi tofauti. Kufanya hivi kunafaida mbili, kwanza, wasomaji wataelewa makusudio na athari yake kitabia itakuwa moja. Pili, utaondoa uhasama na fakachi baina ya watu hasa wanafunzi na kuondoa tafsiri potofu ambayo inatokana na maandishi yanayokubali tafsiri tofauti na kupelekea watu kuwa na fahamu mbalimbali ambazo zinazua hukumu tofauti na kuzua fitina na ugomvi.

### 44. Kukubali juhudi za wengine

Misingi tuliyonayo sio milki ya mtu binafsi kwa hivyo haifai mtu kuona wivu kwa juhudi za wenzake hata ikiwa wao wanatumia mbinu tofauti na jitihadi nyingine. Kile kifaacho ni kuzifurahia juhudi hizo kwani juhudi zetu sote zaingia katika kapu moja na yafaa tuzithamini na kuwapenda waliotekeleza jukumu lao na kuwakhalisia nyoyo na kushirikiana nao kadiri iwezekanavyo. Yafaa pia kuwafaidisha watu kwa juhudi zozote za mtu binafsi au kundi maalumu zenye manufaa hata zikiwa chache au na upungufu na kasoro ndogo.

### 45. Uraia na udini

Wanaolingania katika dini popote walipo wafaa kuihami nchi waliopo na kuhifadhi amani, kuimarisha maendeleo, kuhifadhi mazingira na siku za usoni za nchi. Uhusiano baina ya hisia za kuzaliwa kama vile kujitambulisha na kabila au nchi fulani ni hisia za kawaida ama hisia za hiari kama vile kujiunga na dini au mfumo fulani ni uhusiano wakukamilishana na kushirikiana sio uhusiano wa kupingana na kuvunjana.

### 46. Kudharau usawa na ukweli

Haikubaliki kwa njia yoyote kudunisha au kudharau ukweli au usawa. Ingawa tuna imani na malengo yetu na mbinu tunazotumia kuyafikia malengo hayo, hatudai kuwa mbinu zetu hazina makosa yoyote. Tunapokea na kuheshimu yeyote ambaye atatuonyesha kasoro na makosa yetu kama vile tunaheshimu rai na ufumbuzi wa watu wengine kwa malengo yao mema na mbinu zao nzuri. Cha muhimu ni sote kuwa wakweli na kukhalisi nia zetu kwa Allah na kujitahidi kufanya usawa na kuwa jasiri kutafuta mbinu geni zitakazotatua matatizo yetu na kufikia lengo letu. Kama vile yafaa kuyakubali makosa yetu kwa unyenyekevu na kufurahia kuafikiwa wengine. Jambo hili laonyesha umuhimu wa kubadilishana tajriba. Kufanya hivi kutawaongezea walinganizi ujuzi na elimu na kuwafanya kushirikiana – kupokea kwa wengine na kuwashirikisha – katika waliyonayo. Ni wazi haijapatikana na wala hatapatikana mwanadamu au taasisi iliyokamili, haihitaji nasaha au usaidizi.

**47. Ulokole (Ushupavu)**

Kawaida ya wanaolingania hushikilia mfumo na mbinu mahususi walizozichagua zakufanya da'wa. Kushikilia huku kunatokana na kuona kwao kwamba mfumo ule na mbinu zile ni bora kuliko mifumo mingine na mbinu nyingine. Lakini, ingawa uchaguzi huu umebuniwa kwa elimu, hafai mlinganizi kuona kuwa mfumo wake na mbinu zake ni tukufu zimehifadhiwa na makosa; wala asidhulumu mifumo mingine wala mbinu nyingine. Kushikilia huku bila ya dhulma kunakubalika na kunasisitizwa. Anayekiuka haya anaingia katika ulokole uliokatazwa na dini ya Uislamu na kuuita jahala. Jambo hili lafaa kutukumbusha kuwa aliye bora mbele ya Allah ni yule mchaji Mungu zaidi. Uchaji Mungu unazuia ulokole wa sehemu, kwa mfano mji au wilaya, ukoo, kundi au jamii ya watu fulani.

**48. Mantiki ya kutanguliza ya muhimu kwanza**

Msingi huu unahimiza umuhimu wa kutambua kuwa sio kila kitu katika dini kiko katika daraja moja. Mfano, imani na *tauhidi* ni muhimu zaidi kuliko kuondoa udhia barabarani. Pia vile vile kazi mbali mbali za kulingania haziko katika daraja moja, kwa hivyo yatupasa kuelewa jambo hili vyema na kuweka kila kitu mahala pake. Yahitaji pia kurudia kila mara orodha ya amali za da'wa kulingana na mabadiliko kwani orodha ya amali za Kiislamu haibadiliki lakini ipi itatangulia wakati wa da'wa inategemea hali, wakati na mtu. Yanayofungamana na kutanguliza ya muhimu kwanza ni ujuzi wa kuchagua baina ya madhara tofauti wakati yanatupata ili tuchague madhara yaliyo madogo na ujuzi wa kuchagua faida mbalimbali ili tuchague faida nono.

**49. Kufahamu makusudio ya sheria ya Allah (*al maqaasid*)**

Yafaa wanaolingania kufahamu vyema makusudio ya sheria. Hawafai kushikilia aya na hadithi neno kwa neno na kukomea hapo bila ya kuzingatia makusudi na hekima yake. Mwito huu haumaanishi kuzitupilia mbali nususi (Qur'ani na Sunna) bali wahimiza kuchunguza lengo la aya au hadithi. Pia yahitaji wanaolingania kuzingatia baina ya dalili zilizokubaliwa na wanachuoni wote na zile walizotofautiana na kufahamu masuala kwa kina kulingana na Qur'ani na Sunna. Kupitia makusudio jumla ya sheria na kulingana na msingi "*mwongozo unatokana na makusudio na maana, sio katika maneno wala ibara*," na msingi mwingine, "*mambo hufahamika kwa makusudio yake*". Hakuna shaka kuwa kuuelewa msingi huu vyema hatuna budi kuwauliza wenye elimu katika nyanja hii.

**50. Kufahamu mwisho na athari ya mambo**

Wanaolingania yafaa kuelewa *fikihi* ya matokeo, yaani kuelewa athari ya vitendo wanavyovifanya na maamuzi wanayochukua. Ili kuelewa haya yahitaji ujuzi wa sunna za Mwenyezi Mungu na kuelewa kwa kina yanayojiri katika sehemu, nchi na ulimwengu. Ni wajibu wa wanaolingania kuzingatia matokeo na athari ya jambo juu yao binafsi na wafuasi wao kabla ya kulifanya; na wategemee elimu ya yakini si dhana na wafanye makini bila ya pupa na kufanya mambo kutokana na uwezo wa

kweli sio kubahatisha. Tarehe ya Uislamu inaonyesha vitendo vilivyotokana na uzembe na utovu wa makini, walikusudia wenyewe kuivunja shari au kutenda wema ikawa mwisho wake ni mito ya damu au unyonge wa kudumu.

**51. Kufahamu hali iliyomo**

Kuna haja ya wanaolingania kuwa na ujuzi wa kufahamu na kuelewa kwa kina mazingira wanayoishi ndani yake, uwezo wao, fursa walizo nazo, maadui wao na unyonge wao. Pia yafaa kuelewa masafa baina ya wanayotarajia kufikia, uwezo wao na hali yao kwa sasa. Kuyajua haya kutawasaidia kutambua mbinu na mikakati watakayoitumia inayoambatana na hali zao. Pia vile vile kutambua haya kutawasaidia kuwaandaa watu kiakili na kuwaunganisha katika lengo moja chini ya mikakati iliyowazi na iliyochaguliwa kwa makini na uangalifu kukidhi mahitaji msingi na kutekeleza sunna ya hatua kwa hatua.

**52. Kukuza hisia za kutahadhari**

Umma wa Kiislamu ni Umma unaolengwa tangu jadi kwa kuwa ni Umma uliopokea ujumbe wa Mtume Muhammad *rehema na amani zimshukie yeye* na kuwalingania ambao hawajaupokea ujumbe huo. Kwa sababu hii unaendelea kulengwa na maadui zake, kwani wengi wanaichukia haki. Yafaa kuwafahamisha Waislamu jambo hili na kuimarisha hisia za tahadhari. Bila shaka jambo hili latutanabahisha kupunguza hitilafu baina ya Waislamu na kuleta umoja kwani, sote tumo hatarini na tunalengwa sote. Kutokufahamu hatari hii kunaleta athari kubwa katika Umma, kisha hatari yenyewe imegawanyika sehemu mbili: hatari inayotoka nje inasababishwa na watu wa nje, na hatari inayotoka ndani na inasababishwa na Waislamu au wanaodai Uislamu. Tarehe yetu ni shahidi ya hatari hizi, ingawa hatari ya ndani ni kubwa zaidi na athari yake ni mbaya zaidi kuliko hatari kutoka nje.

**53. Undugu wa Kiislamu**

Undugu wa Kiislamu ni msingi asili miongoni mwa misingi ya Kiislamu na nguzo kubwa miongoni mwa nguzo za da’wa. Kuenea kwake ni katika sababu za kuipata ridhaa ya Allah aliye mbinguni, na kuupata usaidizi wake hapa ardhini na kupotea kwa undugu ni sababu ya kupatikana ghadhabu ya Allah – aliye na uwezo na aliyetukuka – na unyonge hapa ardhini. Ni jukumu la wanaolingania kuvuka sakafu ya kuzungumzia undugu huu na kuupa uhai katika da’wa na watahadhari na chochote ambacho kitauvunja undugu huu. Kutekeleza undugu wa Kiislamu baina ya wanaolingania Uislamu ni chanzo cha kuipokea rehema, bishara yakunusuriwa, na kuipata nusura. Kukosekana kwa undugu huu baina ya walinganizi ni kinyume cha hayo yaani ugomvi, ubinafsi, unyonge na alama ya kuangamia.

**54. Kulingania ni jukumu la wote**

Kulingania dini ya Uislamu ni jukumu la kila Mwislamu na sio jukumu la wanachuoni pekee, ingawa jukumu la kulingania ni zito juu ya wanachuoni kuliko watu wengine. Itakumbukwa Uislamu ni dini ya watu wote, muoga na shupavu, bakhili na karimu, mjinga na mwerevu, na kadhalika. Ama kazi ya kulingania kwa

sababu ya umuhimu wake na uzito wake, inahitaji watu wa tabaka ya juu; watu wenye heshima, mashujaa, wenye subira, wenye maazimio ya kweli, wanaume wa sawasawa, waadilifu, wakarimu; yafaa kuwalea wenye sifa hizi na kuwatanguliza katika da'wa kwani hawa ni fahari wakati wa faraja na tegemeo wakati wa shida. Da'wa inasimama kupitia watu kama hawa na wala haimaanishi kuwa watu aina hii hawana kasoro wala hawakosei. Kila mwanadamu hukosa lakini wao baina ya watu ni dhahabu, wakikosea hurekebisha makosa yao kama vile jua huziba mwezi na yakini kuondoa shaka na kuithibitisha misingi ya haki licha ya kuweka pingamizi na yanayoihatarisha da'wa kuifikisha haki hadi kukutana na Allah katika hali hii. Kila wanapozidi watu sampuli hii katika kazi ya da'wa na kupungua waliopungua daraja hii ni ishara kuwa da'wa inafaulu na kinyume chake ni kweli.

## 55. Hamasa iliyodhibitiwa

Hamasa ni nzuri na ni baraka kwa sababu inaibua maazimio, utendakazi, kutoa, kushindana kwa heri, ukarimu, kuvumbua na kadhalika miongoni mwa sifa nzuri. Hamasa huipa da'wa msukumo wa kupiga hatua kuenda mbele. Kadiri inavyopatikana hamasa, zinapatikana hatua na kadiri inakosekana hamasa inadhoofika da'wa. Kutokana na haya wamezoea walinganizi kuhamasisha watu na jambo zuri wanalolifanya. Lakini yafaa kuzingatia mambo mawili muhimu, kwanza vitendo vinavyotokana na hamasa viwe vimekusudiwa kwa umakinifu; mfano wake ni mfano wa dawa anayomuandikia daktari mgonjwa. Kipimo chake kisizidi wala kisipungue. Hii ni kwa sababu kikizidi kipimo hiki – hasa kwa vijana – kitazua ulokole na hasira huenda zikadhihiri kwa njia isiyokuwa ya sawa. Pili, yafaa mlinganizi mwenye hekima awaandalie wafuasi wake njia za manufaa za kuondoa hamasa zao ili wahisi kuwa lengo lao limenufaika kwani wamefanya waliloweza na kuokoka na hisia zitakazowakumba lau watahisi hakuna manufaa yoyote waliyopata ili wafurahi na kutulia kama vile watu wengine wanafurahia na kunufaika na vitendo vyao.

## 56. Ulinganizi rasmi na ulinganizi wa raia

Kazi ya kulingania inayoendeshwa na vyama na taasisi za serikali ndiyo tunaiarifu kwa ulinganizi rasmi na kulingania kunakosimamiwa na vyama visivyokuwa vya kiserikali tunaiarifu kama ulinganizi wa raia. Imekuwa kawaida – aghlabu ya wakati – kuwa baina ya da'wa rasmi na da'wa ya raia kuna kutoaminiana na kutofahamiana; mara nyingi huwa na hali ya kutarajia kukosana, au kutuhumiana au uadui baina ya da'wa mbili hizi. Mwanzo, lazima kukumbusha mambo mawili muhimu; kwanza, hakuna moja baina ya kambi mbili hizi ambayo ina makosa peke yake au usawa peke yake, kila moja katika kambi mbili hizi ina usawa na makosa. Pili, huenda kambi hizi mbili zikabadilishana afisi, chama rasmi kikawa chama cha raia na chama cha raia kikaingia serikalini. La wajibu ni kila kambi kuweka juhudi na hekima katika kazi yake ili kujenga uaminifu, kufahamiana, kushirikiana, na kusameheana kwani kazi ya da'wa ni jukumu la wote. Likipatikana hili, manufaa yatakuwa mengi zaidi na likikosekana kambi zote mbili, rasmi na ya raia zitapata dhiki na matatizo. Ingawa

ushirikiano huu si rahisi lakini haimaanishi hauwezekani na kwa sababu ya umuhimu wa ushirikiano huu yafaa kuzidisha juhudi ili tufaulu.

**57. Ikhlasi pamoja na kufuata Sunna**

Ikhlasi ina umuhimu mkubwa katika Uislamu, kwani ndiyo kiini cha amali na sharti ya kukubaliwa kwake. Amali iliyokosa ikhlasi imeporomoka bila ya shaka lakini ikhlasi peke yake pia haitoshelezi. Huenda amali imekusudiwa Allah peke yake lakini haikuambatana na mafunzo ya Mtume Muhammad (*rehema na amani zimshukie*). Ingawa kikundi cha *Khawarij* kilikuwa na ikhlasi ya juu, kilijaa makosa mengi na makubwa. Kwa hivyo haina budi da'wa yakulingania watu wawe na ikhlasi iambatane na da'wa ya kutekeleza Sunna, mawili haya (ikhlasi na kufuata Sunna) ndiyo mbawa za uongofu. Kutokana na haya, yafaa wanaolingania kutambua umuhimu wa kuiga Sunna na kuhimiza watu kuifuata kama wanavyo wahimiza kufanya ikhlasi. Hii ni kwa mujibu wa mambo mawili muhimu, kwanza, umuhimu wa kufuata Sunna ambayo ni pacha ya kufaulu, na ni sharti pia, na nusu ya kufaulu. Pili, wengi miongoni mwa wanaolingania ni watu wenye roho za imani na wenye nia nzuri na kwa sababu hii wameteleza na wanateleza kwa kuvutwa polepole, na kudanganywa na kutiwa matatani. Kuna nyakati walinganizi wamejishughulisha na mambo yasiyo muhimu licha ya kuweko mambo muhimu, na wakati mwingine wamejitahidi katika mambo hayana haja na mara nyingine – na huu ni ujinga na upumbavu wa mwisho – wamejitahidi sana na kujitolea kwa wingi katika sehemu ya makosa, wakawa wao ni chanzo cha kuleta mabadiliko badala na kutokomea wao mwanzo na mabadiliko waliyoleta yakawa ni uovu mkubwa kuliko uovu uliokuwa awali.

**58. Upungufu mkubwa**

Utendakazi wa wengi miongoni mwa Waislamu una upungufu na kasoro; walinganizi pia wana upungufu hasa katika shughuli za kidini na kidunia. Jambo hili ni kinyume na vipawa na neema alizowatunuku Allah aliye na uwezo na utukufu zinazowawezesha kuongoza Ulimwengu na kuleta ustaarabu kama vile akida sahihi inayohifadhi haki za viumbe wote, utajiri kwa watu wengi, kufikia cheo muhimu, na maendeleo ya kudumu kwa wanadamu. Yafaa wenye ujuzi kuchunguza tatizo hili ili kuwakomboa Waislamu na uzembe na kuwaingiza katika utendakazi wenye manufaa na kuwatoa katika unyonge na kuwaingiza katika maendeleo. Miongoni mwa yatakayoondoa hali hii ni, kufanya bidii, uvumbuzi, kutathmini, kushindana katika kwa wema, ukamilifu, kuwapa wenye ujuzi nafasi, kazi ya ushirikiano, kuwashajiisha wema, kuwarudi waliokosea na kupenda kazi.

**59. Nadharia ya njama dhidi ya Uislamu**

Mazungumzo yamezidi miaka ya sasa baina ya wanaoitakidi nadharia ya njama dhidi ya Uislamu na wanaoikanusha nadharia hiyo na wengine wasiolemea upande wowote. Ukweli ni kuwa njama dhidi ya Uislamu zilipatikana tangu jadi na zitabakia, lakini haikubaliki kidini na kiakili kufasiri kila jambo kuwa ni njama za maadui. Lazima tufahamu njama hufaulu mara na kuanguka mara nyingine na mara nyingine

huwaangamiza mahasidi wenyewe. Yatupasa sisi kuamiliana na njama hizi bila ya kuchukua mrengo wa kulia au kushoto yaani kupuuza au kutahadhari kupita kiasi kwa kuziweka njama zenyewe mahala pake. Yahitaji tujishughulishe na misingi ya mvutano na kupatana na wenzetu zaidi ya kujishughulisha na utondoti wa mvutano na mapatano. Haifai kuhusisha makosa yetu na kushindwa kwetu na njama zilizoko na zaidi ya haya tusije tukaonjwa kwa sababu ya kughafilika na njama za maadui au kwa sababu ya kuzipuuza au kutahadhari zaidi na kukosa kufahamu jinsi ya kuziepuka njama zenyewe au kwa kupuuza aliyotuamrisha Allah aliye na uwezo na utukufu.

### 60. Duara mbili: duara la uwezo na duara la kushughulisha

Mwislamu ana duara mbili zinamkabili katika maisha yake, ya kwanza ni duara la ushawishi yaani yale aliyo na uwezo nayo ya kujinufaisha mwenyewe na wenzake. Mambo haya analazimika kuyafanya, mfano kuhifadhi siha yake, kujitafutia riziki, kuitunza familia yake na jamaa zake na kuwaongoza walio pamoja naye na kujiendeleza mwenyewe na kukesha kwa ajili ya familia yake na kuelewa kanuni zinazomuhukumu na kadhalika. Pili, duara la mambo yanayomshughulisha kama vile matukio ya sehemu anayoishi na ulimwenguni lakini hana uwezo wa kuyabadilisha kwa njia yoyote, mfano; bei ya sarafu ya dola kupanda au kushuka, uchaguzi wa uraisi wa nchi jirani au mbali, kuchafuliwa mazingira, kupasuliwa kwa tabaka ozoni. Mwislamu mwenye busara anafaa kujishughulisha na kutia bidii katika duara ya kwanza kwa sababu ana uwezo wa kuathiri na kubadilisha na ataulizwa na Mwenyezi Mungu. Ama duara ya pili anapaswa kuamiliana nayo kwa kadiri ndogo ili afahamu yanayojiri ulimwenguni na kuasiliana na wenzake. Ama kuzama na kujishughulisha nayo ataingia katika makatazo na kupoteza juhudi, wakati na nguvu zake katika mambo yakumhuzunisha bila ya uwezo wa kubadilisha na kuendelea kukosa utulivu, na kuhisi kushindwa na kuvaa huzuni na huenda akajitenga na watu na pengine akashindwa kufanya aliyo na uwezo nayo na kujitungia sababu za vitendo vyake na pengine kulaumu kadari kwa anayoyafanya. Bora ya msemo ni msemo usemao "*wanaofaulu ni hodari kutatua matatizo na kuvumbua njia badala, na waliofeli au kushindwa ni hodari kuzua sababu na kutafuta nyudhuru*".

### 61. Umuhimu wa lugha ya Kiarabu

Lugha ni chombo muhimu kibebacho elimu na maarifa, pia ni njia ya mawasiliano na kijenzi kikubwa cha kumtambulisha mtu. Lugha ina sehemu kubwa katika maisha ya watu, na lugha ya Kiarabu ina umuhimu na manufaa kama lugha nyingine isipokuwa lugha ya Kiarabu ina sifa ya kuwa ni lugha aliyoichagua Allah kuwa lugha ya kitabu chake kitukufu. Allah aliye na sifa za ukamilifu – na hekima yote ni yake – anajua zaidi sehemu gani anauteremsha wahyi; wakati wakuuteremsha, sehemu yakuuteremsha, nani atamteremshia, na lugha atakayoitumia. Lugha ya Kiarabu ndiyo lugha ya Qur'ani tukufu na Sunna na elimu ya Uislamu tuliyoirithi. Tarehe ya Kiislamu inathibitisha kuwa kila mara Uislamu ulienea pamoja na lugha ya Kiarabu, Uislamu ulifahamika vizuri zaidi na kuenea zaidi hadi kuporomoka uongozi wa Waislamu wa kisiasa au kudhoofika kwake. Hivi, yatubidi kuifundisha lugha ya

Kiarabu kwa kadiri ya uwezo wetu katika nchi za Waislamu wasiokuwa Waarabu na popote tunapolingania Uislamu.

**62. Kubainisha malengo**

Kila amali ya kulingania ina malengo yake ambayo inawania kuyafikia. Kuyafasili malengo haya ni jambo ambalo lina umuhimu mkubwa na kwa sababu hii yafaa wanaolingania kuchukua muda wa kutosha kubuni malengo yao kwa makini na kuyabainisha neno kwa neno; kuweka wazi maana yake, makusudio yake, umuhimu wake na uwezo wa kuyafikia. Yeyote atakayechanganya – mtu binafsi au chama – baina ya malengo ya mbali na hali yao wakati wa sasa, hadhi yake ya kufeli ni kubwa kuliko kufaulu na huenda akaporomoka. Kosa la mtu binafsi ni msiba lakini kosa la taasisi au chama huwa ni msiba mkubwa zaidi. Miongoni mwa lawama kubwa zinazo elekezwa kwa da’wa ni kuwa wengi miongoni mwa wanaharakati wanajua (wasiyoyataka) lakini hawajui kwa yakini (wanayoyataka). Wakati da’wa inatunga malengo yasiyokuwa sawa au malengo sawa lakini hayawezekani, inajidhuru kwani huwa inakimbiza mazigazi ingawa nia zao ni nzuri hawatayafikia malengo yenyewe. Nia nzuri ni nusu ya yanayotakikana na nusu nyingine ni kuwa sawa, kwa hivyo yapasa wanaolingania kufahamu kwa kina (wao ni nani) na (wanataka nini?) na wabainishe malengo yao kulingana na kujielewa kisha waweke mikakati muwafaka. Hawana budi kuwa wakweli na nafsi zao na wafuasi wao, wakifanya hivyo watakuwa wamefanya wema ama kinyume cha hayo itakuwa balaa.

**63. Ushujaa unaokubalika na usiokubalika**

Ushujaa ni sifa nzuri ambayo yafaa wanaolingania kujipamba nayo kwa kuwa sifa yenyewe ni maandalizi ya lazima katika shughuli ya da’wa. Da’wa haijipambi na sifa ya ushujaa ila ikawa sifa ile ni sababu ya kufaulu kwake na ikivua sifa hii itakuwa sababu ya kushindwa kwake. Ingawa ushujaa ni sifa nzuri, kuna ushujaa wa kulemaza, nao ni ushujaa wa kukaa na kungojangoja na kurudi nyuma wakati wa kufanya uamuzi unaohitajika kwa ukweli, uwazi na kuwajibika. Ushujaa unaotokana na yakini na maazimio ni daraja juu kuliko ushajaa wakukabiliana na maadui kwani shujaa huyu hajali kukosolewa na watu kwani maamuzi yake yanatokana na kuona mbali na amefanya makini na uamuzi wake umeambatana na kukinai. Kurudi nyuma kwa Khalid bin Walid katika vita vya *Mu’ta* ni dalili tosha ya haya.

**64. Cheo na heshima isiyokusudiwa**

Kazi ya da’wa ndiyo kazi bora ulimwenguni katika maisha ya mwanadamu, kwa sababu da’wa ni kazi ya manabii na mitume *rehema na amani ziwashukie*. Ni kawaida-aghlabu ya wakati-kuwa yeyote anayejipamba na sifa yakulingania ataheshimiwa, atapendwa na kupewa cheo juu ya watu wengine. Ni muhimu kwa wanaolingania dini ya Allah wasikusudie cheo wanachokipata kupitia kazi ya da’wa bali wamkusudie Allah katika vitendo na juhudi zao. Wakiheshimika na kupata vyeo bila ya kuvikusudia yafaa wamshukuru Allah kwa fadhila zake na wajihimize kujipamba na sifa za vyeo vile na kuwapenda watu na kuwatendea wema na

kuamiliana nao kwa upole na kuwahudumia na kujizuia kutegemea watu. Yafaa mlinganizi aone daraja na heshima anayoipata kuwa ni jukumu wala si cheo, na dhima sio pambo, na mtihani sio fahari, na jukumu sio ukubwa.

### 65. Wito bali si kazi

Kazi ya da'wa ikibadilika kutoka hali yake ya kuwa wito ikachukuliwa au kufanywa kuwa ni kazi kama kazi nyingine, madhumuni yake hupotea na kubakia sura peke yake. Pia kuifanya da'wa kuwa ni kazi, huleta uzembe na kuondoa nishati na huleta ubinafsi badala ya kujitolea na kuwafanya walinganizi kuwaombea wenye shari na wanafiki, kinyume cha kuwaombea waja wema. Haya yote ni miongoni mwa hasara zinazopatikana kwa daraja tofauti wakati da'wa inadunishwa kuwa ni kazi kama kazi nyingine au kutoka hali yake ya kuwa mwito na kuwa kazi. Natija ya haya ni watu kutokwa na hamu ya kuwa walinganizi, jambo ambalo huwapa maadui wa Waislamu nafasi kubwa ya kuupiga Uislamu.

### 66. Waislamu wapya

Miongoni mwa mambo ya kawaida na yenye kushuhudiwa ni kuwaona Waislamu kufurahia kuongoka watu na kuukubali Uislamu. Lakini mara nyingine furaha hii hupita mipaka na wakaingia baadhi ya Waislamu katika makosa yanayoweza kuepukika. Ili kunufaika sisi na waliosilimu na kuepukana na makosa yanayoweza kutokea yapasa kujua sababu ya msingi iliyomfanya mtu kusilimu, mwangalio wake wa mambo, nia ya kuboresha Uislamu wake, na hekima iliyomuingiza yeye katika Uislamu kisha tumuongoze kwa uadilifu hadi afahamu na kutekeleza Uislamu kwa njia sahihi; kwa nia, fahamu, na tabia. Kuelewa haya na kumuongoza huku kutamlea Mwislamu mgeni pole pole katika dini, ama tukivuka mipaka kwa kuwapokea wanaosilimu-kwa kuwapa mali na mialiko- huenda tukabadilisha nia za wanaosilimu kuwa lengo lao ni kupata mali, au tukamfanya aliyesilimu kujihisi na kudhania yeye ndiye mwalimu na Waislamu ni wanafunzi wake wanahitaji kuelimishwa naye.

### 67. Madhehebu ya kifikihi

Madhehebu ya kifikihi kwa jumla na madhehebu manne yanayofuatwa katika ulimwengu wa Kiislamu hasa ni urithi wenye thamani, na utajiri mkubwa ulioandikwa na wanachuoni na kuhifadhiwa na kuboreshwa na wakati. Madhehebu haya ni fahari ya Umma wa Kiislamu, na Mwislamu afaa achague madhehebu atakayoifuata. Lakini ni bora afahamu – kadiri ya uwezo wake – dalili zinazotumika katika madhehebu yake na aheshimu rai na hukumu tofauti za madhehebu nyengine na kunapokuwa na haja ya kuzungumzia hitilafu baina ya madhehebu moja na nyingine basi mazungumzo hayo yawe ya adabu na lengo lakudhihirisha haki na kuifurahia haki hata ikitoka katika ulimi wa madhehebu tofauti. Hakika kila madhehebu ya kifikihi ina usawa na makosa, na hukumu zinazokubalika na zisizokubalika, jambo hili ni jambo lililokaririwa na wanachuoni wakweli wakubwa walio na uwezo wa kupima baina ya madhehebu zote na kuona hukumu ipi iliyo sawa na ipi ilikosa.

Ama ulokole wa madhehebu moja unadhuru zaidi, lakini pia kudharau kufuata madhehebu na kuyapiga vita na kuwalingania Waislamu kuwachana na madhehebu na kushikamana na Qur'ani na Sunna moja kwa moja ni madhara makubwa zaidi. Mwito wa kuzuia watu kufuata madhehebu ni jambo lisilowezekana kivitendo, kisha wanaopigia debe mwito huu na kuhimiza watu kushikamana na jitihadi na fatwa wanazozichagua wao au zilizochaguliwa na mashekhe wao hawafanyi jingine ila kupanda mbegu za madhehebu nyingine ya *fikihi* – kwa kukusudia au bila ya kukusudia - na kufanya hivi ni kinyume na mwito wao wa kuyapinga madhehebu.

## 68. Mwanamke wa Kiislamu

Mwanamke wa Kiislamu anapata shida kubwa kutokana na dhulma inayotokana na pande mbili hasimu; kwanza, waliopuuza dini na kuendesha mambo nje ya misingi ya dini wanakwenda mbio kumvua mwanamke wa Kiislamu dini yake, utu wake, heshima yake na uke wake. Pili, waliopita mipaka ya dini na kumvua mwanamke wa Kiislamu uhai, kumfanya kama sanamu, kumzuia kutoa mchango wake katika maisha. Wanaoshilikia mrengo huu wa pili ingawa wana nia nzuri hawaepuki lawama. Kumdhania mwanamke wa Kiislamu, kumshuku, kumdharau na kuuchukulia uongozi wa mwanamume kwa njia isiyofaa yatokana na kutofahamu haki za mwanamke katika Uislamu na umbile lake na kuzitanguliza ada na desturi zilizoenea kwa muda mrefu mbele ya dini. Kufanya hivi hudhihirisha ada na desturi kana kwamba ni miongoni mwa dini licha ya dini kuwa mbali na desturi hizo.

Yafaa Waislamu kwa jumla na wanaolingania hasa kuwaamini wanawake, kumpa haki zake na kumuandaa vyema ili achukue nafasi yake katika maisha na fursa ya mwanzo katika nafasi hiyo ni haki ya mwanamke kutekeleza da'wa. Kufanya da'wa kwa mwanamke kuna faida nyingi miongoni mwa faida hizo ni, kuhakikisha uadilifu na uadilifu ni msingi muhimu katika Uislamu, kufaidika na juhudi zake katika da'wa hasa zaidi katika nyanja ambazo mwanamke anafaa zaidi kuliko wanaume. Pia yafaa kuzirudi sauti zinazodai kumkomboa mwanamke kwa kudai kuwa amedhulimiwa hivi au vile. Hakika Uislamu umemkomboa mwanamke na kumpa cheo chake cha sawa, cheo chenye uadilifu, kinachoambatana na uke wake, kuhifadhi haki zake, heshima yake, uhuru wake, asili yake, na utu wake na kumfanya yeye ni kiungo nusu katika jamii, na wa pili wa mwanamume na mwenye kulea kizazi.

## 69. Maana ya ibada

Lengo msingi na kubwa zaidi la kuwepo wanadamu katika ardhi hii ni kumuabudu Allah aliyetukuka aliyesema

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

> *"Sikuwaumba wanadamu na majini ila (kwa ajili) waniabudu*"[Ad dhariyat, 51:56].

Fahamu hii kamili ya neno ibada inamfanya mwanadamu kumtii Mola wake zaidi na kuwa na furaha kila wakati kwa uhusiano wake na Mola wake na kuwanufaisha viumbe na nchi. Kwa bahati mbaya watu wengi wamepoteza fahamu hii pana ya ibada na kubakia na vitendo dhahiri pekee na vitendo hivi vimebakia ndio ibada peke yake.

Jambo linalofaa kuwekwa wazi kwa wakati huu ni kuwa ufafanuzi na kugawanya amali za kidini; akida, ibada, kuamiliana na watu ni ufafanuzi wa kielimu ulioambatana na haja ya kuelimisha na kuwafahamisha watu. Lakini kuelimisha huku kulipelekea baadhi kufafanua ibada kwa maana finyu, kosa ambalo lilieneza maana finyu ya neno ibada kwa upande mmoja na upande mwingine kudhihiri baadhi ya vitendo mahususi kuwa ndio ibada na vingine kuwa ni ada. Kutokana na kosa hili yafaa kufahamisha watu maana sahihi ya ibada ili ikusanye kila jambo miongoni mwa akida, siasa, ibada dhahiri, kuamiliana na watu, kuishi, kulingania, kujifurahisha kwa njia ya halali, kujipumbaza, kuboresha kazi, kutenda wema na kadhalika.

### 70. Kuelekea mbele

Allah anaumiliki wakati katika hali ya kuendelea bila ya kusimama. Wakati uliopo ni mwana wa jana na mzazi wa kesho. Kwa hivyo yapasa kazi ya da’wa inufaike na tajriba ya waliotangulia na kuamiliana vyema na waliopo na kujiandaa kwa kesho. Yafaa Mwislamu kutekeleza yanayofaa ili kujiandaa kwa kadiri ya uwezo wake kisha kumuachia Mola wa viumbe kwa kumuamini, na kumtegemea kwani kuangalia mbele na kujiandaa ni wajibu wa kazi ya kulingania na alama ya kuongoka na sababu ya kufaulu. Anayefanya hivi huwa ametenda wema na asiyefanya hivi basi hujihukumia kuganda katika hali moja na kujiondoa kisha hubakia kuwa ni hadithi za kusimuliwa alifanya aliyofanya na kukunjwa katika jamvi la wakati. Uislamu ni dini inayoangalia mbele; tunayapata haya katika mambo mengi ya kidini muhimu kati ya hayo ni kuhimiza kuchunga mipaka ya Allah na kujiandaa kwa siku ya malipo kwani makao yetu ya kweli ni huko. Wengi wanakifahamu kisa cha Nabi Yusufu alipowaokoa wana wa Misri kutokana na baa la njaa lilowakabili kwa miaka saba kwa kujiandaa kuipokea miaka ya njaa. Mtume Muhammad *rehema na amani zimshukie* alikuwa akijiandaa kwa mustakabali kwa makini na utondoti katika kila jambo. Dalili ya haya ni kugura kwa masahaba kwenda nchi ya Uhabeshi na kugura mara ya pili kwenda mji wa Madina na mkataba alioandikiana na Mayahudi, na majeshi aliyoyatuma, na vita alivyopigana, na barua alizotuma, na ufahamu wake wa habari za ulimwengu, na kuelewa kwake idadi ya Waislamu wa Madina, na mengineyo yaliyoko katika sera ya Mtume *rehema na amani zimshukie yeye*.

### 71. Mjibizo

Baadhi ya waja wema wanaolingania wanafaa kutahadhari kukabiliana na makosa yanayopatikana katika jamii kwa kuvuka mipaka au kuwatia watu katika dhiki ilhali dini imetoa nafasi katika jambo husika. Imamu Muhammad Abdu alihofia athari ya hali ya kubakia nyuma iliyoenea sana katika jamii kwa upande mmoja na kuenea kwa itikadi potofu kwa upande mwingine; jambo hili lilimfanya kuhimiza thamani ya

kufahamu na kutumia akili. Naye mshairi Muhammad Iqbal alikuwa na huzuni kwa kushuhudia kuzembea kwa Waislamu na kushindwa kujitahidi katika mambo yao kwa mujibu wa fahamu yao potofu kuhusu *qadhaa* na *qadar* naye akahimiza watu kuelewa uweza wao wakubadilisha hali zao. Mfano wa nasaha hizi pia zinaelekezwa kwa wanaofahamu makosa maana ya bid'a kwa kuipanua maana ya bid'a na kuchukulia kuwa bid'a potofu zimeingizwa katika dini licha ya dini kuwa mbali na uzushi. Pia vile vile wanaopinga ulokole wa madhehebu ya *kifikihi* na kuwaita watu kuachana na madhehebu na wanaoshuhudia utajiri katika sehemu fulani wakaamua kuyakimbia maendeleo na utajiri kwa madai ya kuwa wanafanya *zuhudi* (kuipa maungo dunia). Kukabiliana au kujibu vitendo na matamshi au hali fulani haifai kwenda kinyume na dini au kukia mipaka ya dini.

## 72. Ushindi na kushindwa

Tarehe ya Uislamu imejaa mashujaa na Waislamu wenye ujasiri mkubwa wanaotupa sisi kama Waislamu fahari kubwa, pia katika tarehe ya da'wa watu sampuli hiyo na shupavu wanaipa kazi ya da'wa fahari. Ingawa mashujaa hawa wananufaisha kazi ya da'wa kwa kuwa mfano bora na kielelezo cha kuhamasisha utendakazi, mashujaa hawa huenda wakawa athari mbaya ikiwa da'wa itawatumia kujifakhiri na kuimba imba sifa zao bila ya kuathirika nao. Hukumu hii pia inafaa kutumika kwa wale ambao wanajifakhirifakhiri na tarehe ya Uislamu na kujigamba na waliopita na yaliyopita bila ya kuathirika nayo.

Waliotangulia, na tarehe pia, inasimulia makosa yaliyotokea baina ya Waislamu, makosa haya yafaa kuwa somo na sababu ya kuhamasisha jitihada murua na utendakazi. Makosa haya ikiwa yatabakia, ni sababu ya huzuni na kulimbika lawama kwa watu au kundi fulani na kujiadhibu kwa kujipiga, yatakuwa ni madhara matupu leo na siku zijazo.

## 73. Kufadhilisha uhai

Kuuliwa kwa ajili ya Allah ni cheo kikubwa anachowatunuku waja wake wema; daraja hii inakusudiwa na wengi lakini uhai katika njia ya Allah ni sawa na mauti katika njia ya Allah. Ingawa jihadi ni nzuri na inafaa, huenda kubakia hai katika njia ya Allah kuna manufaa zaidi kuliko *shahada* (kuuliwa katika njia ya Allah) hasa ikiwa wanaolingania watatumia mbinu na juhudi zao zote kuimakinisha dini na kuuhudumia Umma na kuwa mfano mwema kwa Waislamu ili kuwavutia wasiokuwa Waislamu kusilimu.

## 74. Maasia na taa

Roho na viungo vya wanadamu vinajihusisha na twa'ta na maasia, na vitendo vya roho vina umuhimu juu ya vitendo vya viungo kwani roho ndiyo kiini cha mwanadamu. Roho pia vilevile ndiyo inashawishi na kuhukumu vitendo atakavyo fanya mwanadamu viwe vitendo vya taa au maasia. Kuepukana na maasia ya roho ni vigumu kuliko kuepukana na maasia ya viungo kama vile kuisimamisha roho katika taa kuna ugumu kuliko kusimamisha viungo katika taa. Yampasa Mwislamu kujizuia

na maasia ya kiroho na kivitendo na kusimamisha taa kamili. Kufanya hivi kutampa mja mizani inayotakikana baina ya dhahiri ya jambo na hakika yake, na baina ya sura na madhumuni na baina ya nia nzuri na vitendo dhahiri.

## 75. Kushikamana na dini kunakokubalika na kusikokubalika

Kushikamana na dini kwa njia sahihi ni kuwa na akili pevu na roho iliyosalimika na magonjwa; mwenye sifa hizi huwa ni mtu mwenye bashasha baina ya watu na mfano unaopendeza na kuvutia. Ingawa yafaa kushikamana na dini, yafaa kutahadhari kwenda kinyume na sifa za dini inayotokana na fahamu duni au magonjwa ya roho kwa pamoja, au moja ya kasoro hizo mbili. Aliye na fahamu pungufu ya dini huchukiza na kuchukiwa na watu; udini wa aina hii ulikuwa na waendelea kuwa pingamizi ya Uislamu na athari yake ni mbaya kuliko athari ya maasia katika jamii ingawa wanaohusika hawaoni hasara yake juu ya dini. Alama ya udini huu ni kuboresha dhahiri bila ya undani, na kutokujali na kiini na madhumuni na kuhimiza yasiyo lazima na kuacha ya lazima, na kushughulika na maslahi ya nafsi badala ya maslahi ya jamii. Katika alama za udini pungufu pia ni mtu kuvisha hawaa na upungufu na unyonge alionao mwenyewe vazi la dini na kupigania cheo asichokuwa nacho na kuwavunja na kuwakosoa walio na cheo kwa uhodari na uweza wao.

## 76. Hadithi zinazozungumzia misukosuko, vita na mauaji

Uislamu ni dini iliyohifadhiwa na yenye kunusuriwa na Allah aliye na uwezo na utukufu; ushindi ni wake hata wakichukizwa maadui wa Uislamu. Haya ni kwa mujibu wa Qur'ani na Sunna na bishara za wakati wa sasa na makisio ya siku za usoni. Yakini ya ushindi huu, yafaa kupatikana kwa wanaolingania bila ya shaka yoyote kwa kuwa ni ukweli, mwanzo, na pili yakini hii inawapa motisha kujitahidi zaidi na kuwavutia wengine kuinusuru dini hii.

Jambo ambalo lafaa kutajwa hapa ni kuwa hadithi nyingi zinazozungumzia vita na mauaji ni hadithi dhaifu na zilizokuwa sahihi miongoni mwa hizo na kuzungumzia kuwa Umma huu utapatikana na matatizo mengi yatakayozidi zama baada ya zama ni matukio mahususi ya wakati maalum, au sehemu maalum, au mtu maalum, jambo ambalo linaondoa sifa ya yakini ya matukio yenyewe. Kuzichukulia hadithi hizi kwa ujumla na kufahamu kuwa matukio yenyewe yatakuwa ni mambo ya kawaida wakati wote na sehemu zote ni kosa kubwa kwani fahamu hii ni kinyume na dalili thabiti na wazi za kisheria zinazobashiria ushindi wa Uislamu kama vile fahamu yenyewe inakwenda kinyume na Sunna ya Mwenyezi Mungu katika ardhi, pia inakwenda kinyume na matukio ya tarehe zamani na zama za sasa; vile vile fahamu inahalifu uadilifu wa Allah aliye na uweza na utukufu. Ametakasika Allah kuwakalifisha watu kuinusuru dini hii na kuwaahidi ushindi ilhali hawanabudi ila kushindwa. Wakati itafahamika kuwa dalili mahususi hufahamika kupitia dalili jumla na dhana haivunji yakini; tutazichukua hadithi zinazozungumzia *fitna* (misukosuko, vita na mauji)

mahala pake na kubakia na yakini kuwa Uislamu ni dini inayonusuriwa kwa amri ya Allah Muweza.

### 77. Utajiri na starehe

Utajiri ni chanzo cha ufisadi unaoharibu maisha ya mwanadamu. Kwa sababu hii Uislamu umekataza starehe bila mipaka na kutahadharisha kuwa kuenea kwa utajiri unaokia mipaka ya Allah baina ya Umma wowote, ni alama ya kuangamia kwake. Kwa sababu hii wanaolingania wafaa kupambana na starehe nyingi inayowapeleka watu kumuasi Allah na wanawajibika walinganizi kuzuia misingi ya starehe aina hii. Ingawa utajiri unaoleta starehe nyingi una hatari, baadhi ya starehe hizi zina hatari kuliko nyingine na inawajibika kwa walinganizi kupambana nazo. Mfano wa utajiri hatari ni starehe ya kuwa na akili na wakati kwa baadhi ya wanaolingania au wanaodhania kuwa wao ni walinganizi, kutumia wakati wao kusoma na kuandika kuhusu vikundi au madhehebu yaliyokufa na kusahaulika. Vikundi hivi au madhehebu haya, hayaathiri Umma wa Kiislamu kwa njia yoyote; yashuhudiwa baadhi ya waandishi, wakiandika mlango mzima au kitabu kizima kuyahusu makundi au madhehebu yaliyosahaulika. Anayesoma makala au vitabu hivi hafahamu lengo wala makusudio ni nini. Waandishi wengine wanaandika habari zisizokuwa na muelekeo wowote na mara nyingine habari zile hazina ukweli, kwa lengo la kuwavutia wasomaji na kudhihirisha fahamu yake pana. Wengine wanaandika maneno yasiyofahamika; jambo ambalo latokana na fahamu finyu ya analokusudia kubainisha au anahofia kueleza wazi mawazo yake kwa sababu moja au nyingine. Mifano hii na mingine ni aina ya utajiri wa akili unaoleta starehe ya kufikiria na kutumia juhudi kwa mambo yasiyo na faida na utajiri huu unafanana na utajiri wa mali na huenda ukawa mbaya zaidi. Yafaa kuwatahadharisha walinganizi waadilifu na wenye ikhlasi, kwani kujishughulisha na mambo kama haya ni kupoteza wakati, mali, juhudi na thawabu na kuyakimbia majukumu asili. Huenda utajiri huu ni kishawishi na mtego, au kujipurukusha au njia ya kuwashughulisha walinganizi ili wasishughulikie yaliyo muhimu kwa njia moja au nyingine licha ya kuwa kupatikana nia nzuri katika utajiri aina huu hauondoi lawama kwa wanaohusika.

### 78. Dini ya *tauhidi* na umoja

Uislamu ni dini ya *tauhidi* na dini ya umoja. Umma wa Kiislamu unampwekesha Allah na kuungana pamoja katika dini na kwa sababu hii walinganizi wafaa kutanguliza kuwaunganisha Waislamu kimawazo, hisia, na vitendo na yafaa pia kutahadharisha Waislamu kutengana kimawazo, hisia na vitendo. Umoja ni nguvu, na chanzo cha kuipata rehema, baraka na nishati ya kazi pamoja ya kuwa ni sababu ya kuipata nusura ya Allah na kutengana ni kinyume cha haya yote.

Ingawa kazi ya da’wa ina matunda makubwa na athari nzuri kwa Umma wa Kiislamu na ni kielelezo cha hamu na ghamu wanazopitia Waislamu na matamanio yao, da’wa peke yake haiwezi kutimiza malengo ya Uislamu.

Hali hii inatokana na sababu kadhaa; ya mwanzo katika sababu hizo ni ukosefu wa umoja katika da'wa ambao mara nyingine hufikia chuki na uadui. Miongoni mwa yatakayoleta umoja unaotakikana au kuukaribia umoja, ni ikhlasi na kueneza mahaba na kuacha mijadala kuhusu masuala madogo madogo katika akida na *fikihi*; walitofautiana waliotutangulia na waliokuja baada yao na wanachuoni walioafikiwa kuipata haki katika tofauti hizo, wana thawabu na waliokosa wamesamehewa.

### 79. Kutofautiana kuliko na manufaa

Miongoni mwa makosa baina ya walinganizi wengi ni mawazo na hisia kuwa wanaosimama dhidi ya Uislamu ni safu moja na umoja wao huu unadumu kila wakati. Ukweli ni kwamba maadui wa Waislamu hawana umoja wa kudumu bali huungana katika jambo moja na kufarikiana katika jambo jingine na mara nyingine baadhi huchukua misimamo inayosaidia Waislamu na Uislamu bila ya kuangalia nia zao. Kwa hivyo yafaa Mwislamu kuwasoma wanaosimama dhidi ya Uislamu na kuelewa kwa kina tofauti zilizoko baina yao na kutumia tofauti hizi kwa manufaa ya nchi na waja. Ama kosa la kujumuisha mahasimu wote pamoja ni kinyume na Sunna ya Mwenyezi Mungu, na ni kinyume na matukio ya tarehe na zama za sasa. Kujumuisha huku ni uzembe wa akili na uvivu wakuzingatia na kunufaika na nafasi zinazojitokeza baina ya tofauti hizi. Pia vile vile kutozingatia tofauti hizi ni kujidanganya wenyewe na kujipa nyudhuru kuwa walinganizi na Waislamu hawana lawama kwa uvivu na uwoga wao kwa dhana kuwa wanakabiliana na nguvu wasizoziweza kwa madogo na makubwa.

### 80. Kutekeleza sheria za Allah

Swala muhimu linalotaka jawabu ni; vipi tutatekeleza sheria ya Allah katika nchi zinazohukumiwa kwa hukumu isiyokuwa ya Allah ili zirudi katika hali yake ya uongozi wa sheria na kuwa kielelezo chema? Mwanzo hakuna mwenye akili anayedai kuwa kuna njia au suluhisho moja linalofaa katika kila wakati na kila sehemu. Huenda tatizo hili likatatuliwa kwa njia ifuatayo. Ni wajibu wa walinganizi kuendelea na juhudi zao za kudai utekelezaji wa sheria kwa njia ya amani, wazi na kudumu. Pia inawapasa kuwahamasisha watu wote kuhusu haki yao ya kuhukumiwa na sheria ya Allah na wajibu wao kuhusu kudai kuhukumiwa na sheria. Miongoni mwa faida za njia hii ni kuondoa au kupunguza wasiwasi na uoga wa viongozi, jambo ambalo lina faida kwa walinganizi wenyewe na viongozi au serikali; pia huenda serikali na viongozi wakaathirika na kutenda wema kutokana na nafsi zao, athari ambayo haipatikani kwa kushindwa kwa walinganizi kutekeleza jukumu lao, au njia isiyokuwa sawa au khofu. Faida nyingine ni kupatikana utekelezaji wa sheria hatua kwa hatua, kinyume na hali ya mtaka yote hukosa yote wakakosa walinganizi kila kitu. Na faida nyingine ni kutowapa maadui, mahasidi na waovu njia ya kuharibu mwito wa kutekeleza sheria kwa kutumia harakati za kupigania sheria kwa kuwa madai yenyewe yamechukua mfumo wa amani.

Pia faida nyingine ni kuweza kujitathmini, kwani uwazi wa mfumo huu utadhihirisha makosa kinyume na harakati za siri. Ni wajibu wa walinganizi kupigana na nafsi zao dhidi ya kupenda ukubwa na uongozi na watangaze kwa wazi na ukweli kuwa hawapiganii sheria ili wapate wao uongozi, wao ni wasaidizi wa yeyote atakaye hukumu kwa sheria ya Allah. Kufikia hapa yapendeza kutaja maneno ya hekima aliyokuwa akiyakariri Shekhe Abu Al Hassan An Nadawi, "*Ni bora imani iwashukie wenye mamlaka kuliko mamlaka yawashukie wenye imani*". Nasiha hii njema ina sifa za ufunuo na kuafikishwa na Allah aliyetukuka na inafaa walinganizi wote kuiweka maanani daima na kila sehemu kwani utekelezaji wa sheria hautimu ila baada ya wananchi wengi kua na imani nayo bila ya vita au kulazimishwa.

### 81. Bali wataulizwa

Walinganizi wengi wanadhania kuwa hawataulizwa kuhusu matokeo ya juhudi zao za kulingania hasa wakati wameshindwa kufikia lengo la da'wa; fahamu hii inahitaji kudhibitiwa kwani kuiacha bila ya kuibainisha kuna hatari kubwa. Ndogo ya hatari hii ni kuwacha kutathmini utendakazi wa walinganizi na kuwachukulia walinganizi wote kuwa sawa; weliojitahidi na kutenda wema na waliozembea na kukosea. Hakika walinganizi wakimkusudia Allah na kuitafuta haki na kujitahidi kadiri ya uweza wao kisha wakafaulu wana shukrani na malipo mema na wasipofaulu wanasamehewa lakini ikikosekana moja ya sharti tatu hizi (ikhlasi, kutafuta haki na kujitahidi kadiri ya uweza) au zaidi, haina budi kuporomoka rajaa yao na wataulizwa kuhusu kushindwa kwao.

### 82. Wema usiokuwa mwema

Muumini akiidhibiti nafsi yake juu ya taa na kujiepusha na maasia husifika,t na ni ishara ya tohara ya roho yake na ukamilifu wa akili yake na mfano wa kweli wa *tawakul* yake na yakini ya kweli na dini anayoilingania. Lakini huenda muumini akateleza na kukosa kwa kujiona yeye ni bora kuliko anaowalingania. Kiburi hiki chatokana na nafsi kujidanganya na athari yake ni mlinganizi kujitenga na anaowalingania ili utukufu wake usichafuliwe na maasia yao, na elimu yake kwa ujinga wao, na cheo chake kushushwa na watu wa chini. Akifika mtu daraja hii hawi mlinganizi kwa madogo au makubwa bali huwa ni mzigo kwa da'wa. Yafaa walinganizi kuwa juu na mbali na batili, sio juu ya wafuasi wao bali anawajibika mlinganizi kumshukuru Allah kumtunuku cheo cha kuwahudumia Waislamu, cheo ambacho kinafundisha kuwapenda anaowalingania, kuwasubiria na kuhamasisha wema walionao. Kufanya hivi atakuwa mlinganizi ametumia cheo na wema wake mahala pake na akaepuka na ugonjwa miongoni mwa magonjwa ya nafsi. Hakika hiki ni cheo cha haki na misingi thabiti, sio cheo cha mtu na kikundi.

### 83. Uraibu wa kesha tupu na hatari

Miongoni mwa magonjwa ya nafsi pia ni mikutano ya baadhi ya walinganizi katika vikao tofauti, iliyokaribu na kesha tupu isiyokuwa na faida kuliko kuwa karibu na amali yenye faida. Walinganizi hawa hukesha wakazungumzia kuhusu hili na lile na

kumkosoa mtu fulani na kikundi fulani na kuporomosha hasira zao juu ya jambo au kitu fulani kisha wakazungmzia matarajio yao na kutumia muda mwingi katika matamanio haya na mwisho wa haya yote wakatawanyika bila ya kutenda lolote au kuamua kutenda lolote kisha kujihisi hawana lawama mbele ya Mola wao. Kwani kwa kufanya hivi wameinusuru dini kwa uweza wao ilhali hakika ya jambo ni kuwa hawajainusuru dini kwa lolote wala chochote bali wamedanganya nafsi zao kwa kupiga domo mara kwa mara, kutupa wakati na kuridhisha matamanio yao ya mazungumzo. Kufanya hivi ni kudhihirisha kwa urongo hisia zao za kuihudumia dini; wanadanganya nafsi zao baadhi yao wao kwa wao na kubadilishana vikombe vya ridhaa na kuondoa kiu na hamu ya kufanya lolote. Kwa kufanya hivi wao hukimbia wajibu wao msingi na kuvisha unyonge wao, kushindwa kwao, na domo lao vazi la dini wasiyokuwa na haki nayo kwa mafupi wala marefu.

## 84. Wastani na uadilifu

Uislamu ni dini ya wastani na uadilifu na iko mbali na pande mbili zilizovuka mipaka; imani kali na kudharau na kupuuza dini. Allah amewasifu Waislamu kwa kusema

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطًا لِّتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ

*"Na vivyo hivyo tumekufanyeni umati bora (kama kibla chenu tulivyokifanya bora) ili muwe mashahidi juu ya watu"* [Al baqara, 143].

yaani bora na waadilifu kwani bora ya mambo ni yenye kuwa kati na kati, ulokole na kuipuuza dini hayakubaliki.

Wastani wa Uislamu unadhihiri katika nyanja zote za maisha kwa mujibu wa hekima iliyowazi, kwani hii ni dini kamili na ya mwisho. Mwislamu haupi uhai mgongo kiasi cha kwenda kinyume na maisha na kujitahidi kujikimu kimaisha kisha akawa mzigo kwa wenzake, pia hafai kuzama katika maisha na hamu yake kubwa kuwa ni kukusanya mali. Yafaa atafute riziki kwa kipimo, kama vile kipimo hiki kinatumika katika maisha na kutafuta riziki pia kipimo hiki kinatumika katika ibada, kutoa, kuamiliana na watu, mavazi, na kupima baina ya maslahi ya mtu binafsi na maslahi ya watu wengi, na baina ya haki na wajibu, na baina ya roho na mwili, akili na nafsi na kadhalika bila ya kuvunja mipaka au kuipuuza. Hakika kuvuka mipaka ni jambo lisilokubalika kwani hupoteza maslahi ya mtu na jamii na kupuuza dini haikubaliki kwani ni kinyume na umbile la mwanadamu. Kwa sababu hii imani kali ilikuwa na itabakia kuwa sababu msingi na mbegu ya kujiangamiza na kwa minajili ya haya Allah aliyetukuka akachagua dini ya Uislamu iwe ni dini ya wastani na kati na kati kwani Allah amemuumba mwanadamu na kumkalifisha nayo na Allah ni Mjuzi wa umbile la mwanadamu na uweza wake na udhaifu wake.

## 85. Tofauti na hitilafu

Uislamu hupata nguvu na kuendelea kupitia umoja na Uislamu umesisitiza kupatikane umoja na kutahadharisha tofauti na kukatana. Lakini pamoja na kuhimiza umoja,

Uislamu unakiri tofauti za kawaida baina ya wanadamu ambazo lazima zilete kutofautiana baina ya watu, jambo ambalo ni Sunna ya Mwenyezi Mungu katika viumbe vyake. Hitilafu ziko aina mbili; hitilafu yenye manufaa na hitilafu yenye madhara, ama hitilafu yenye manufaa ni hali ya kutofautiana katika rai kwani tofauti hii huongeza hazina ya tajriba ya wanadamu na inaambatana na umbile la mwanadamu kulingana na hekima ya Mola. Ni makusudio ya Allah – aliye mbali na kasoro ya aina yoyote – kuwaumba wanadamu tofauti, kiakili, fahamu, na njia za kufikiria kama vile tofauti ya tabia, rangi, na maumbile ni dhahiri shahiri. Ama hitilafu yenye madhara ni kutofautiana kwa nyoyo ambako Allah amekataza kupitia aya tukufu na hadithi sahihi; mfano wa aya hizo ni

وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا ۚ

*"Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu nyote wala msiachane"*
[Aali Imran, 103].

Hakika ya hitilafu inayofaa ni kutofautiana kwa rai zisizopingana bali zenye kukamilishana mfano wa mshumaa; ukiasha mishumaa mingi utaongeza mwangaza na kila ikizidi idadi ya mishumaa nuru huongezeka, na mshumaa mmoja hauathiri mshumaa mwingine. Ama hitilafu yenye kudhuru ni kutofautiana kwa rai zenye kugongana ambako kunazua ushindani, ushabiki na uadui na kudhoofisha wote hadi ikaondoka nguvu yao na sura yao.

Ingawa kuna kutofautiana kwa haki au batili, kuna mambo katika dini ambayo hayakubali tofauti ya aina yoyote kwani mambo hayo ni misingi thabiti na ndio dini. Misingi ambayo inahifadhi dini na ndiyo lengo lake na viunganishi vya akida, mwenendo na hisia. (Viunganishi hivi ni akida, ibada, tabia, na hukumu zisizobadilika). Viunganishi hivi vyaonyesha umuhimu wa kusoma *fikihi* ya hitilafu na adabu za kutofautiana na kukubali haki za wengine kuwa na rai tofauti maadamu ni rai inayokubalika katika sheria, mfano wa haya ni hitilafu kuhusu suala la kutumia njia na mbinu zinazotofautiana kulingana na hali, wakati na mahala.

### 86. Kujificha

Kuna Waislamu ambao hujificha nyuma ya tarehe ya Waislamu wema na uzuri wa dola za Kiislamu zilizotangulia na kuzungumzia haya kwa wingi na kuimba sifa za Waislamu na Uislamu wa wakati huo na kujinasibisha na wakati huo bila ya kufanya chochote au lolote katika yale anayo uweza nayo kwa kudhania kuwa akifanya hivyo amejitoa katika majukumu yanayomkabili. Na kuna wale wanaojificha nyuma ya dhiki na hali ngumu wanayopitia Waislamu wa leo na kuzidi kuzungumzia suala hili na kusikitika na kulaumu na kulaani - kwa haki au batili- kundi au chama hiki au kile bila ya kufanya chochote au lolote katika yale anayoweza kwa kudhania kuwa kwa lawama na kilio chake ametekeleza jukumu lake. Kikundi cha tatu ni kile kinakimbilia kujificha nyuma ya siku za usoni kwa hivyo hawafanyi lolote kutegemea kuja kwa Imam al Mujadid (atakayeleta mabadiliko) au Al-Mahdi anayesubiriwa, au

kiongozi mchaji Mungu, au hodari mtekelezaji kwa matarajio kuwa kuja kwa mmoja katika hawa itakuwa ni suluhisho la matatizo yote na kupatikana yote yaliyotamaniwa bila ya kuzingatia Sunna au misingi thabiti na kanuni zisizobagua na desturi ya mambo.

Aina tatu hizi za watu hakika wanakimbia majukumu yao na kutenda wanayoweza kwa kadiri ya uwezo wao na kubuni nyudhuru zisizokubalika kwa kushindwa kwao na kudanganya nafsi zao nao ni kizuizi katika kazi ya da'wa na mzigo katika maisha. Ni juu ya Mwislamu kufahamu da'wa yake, ulimwengu wake, na afahamu anayoweza kuyafanya kisha ayafanye kwa ikhlasi na kwa uhodari yawe madogo au makubwa. Kidogo kidogo huwa kikubwa na tone na tone huwa bahari. Allah akiziona ikhlasi za waja na ukakamavu wa kuboresha utendakazi wao ataikubali kazi ile na kuikuza hata ikiwa ndogo kisha ukafaulu Umma kwa matunda mazuri na amali njema.

## 87. Kuamiliana na *fitna*

Mara kwa mara hutokea *fitna* au matatizo au kubabaishwa Waislamu kama vile kumkufuru Allah, kumtukana Mtume Muhammad *rehema na amani zimshukie* au kuvamiwa Waislamu wa nchi fulani, au sehemu tukufu au kitu kitukufu miongoni mwa vilivyotakaswa na Uislamu, au kukejeli moja katika misingi ya Umma na kadhalika. Nia na malengo yanayowafanya maadui kuuhujumu Uislamu na Waislamu zinatofautiana; miongoni mwa sababu hizi ni chuki, uadui, ujinga, kutaka umaarufu, kushughulisha nguvu na juhudi za Waislamu kutoka uwanja wa vita na kutawanya juhudi zao na mali yao katika vita mbali mbali.

Yafaa akili ya da'wa iweze kutofautisha nia na sababu zinazozua *fitna* na misukosuko baina ya Waislamu na kuamiliana na *fitna* hizo kulingana na sababu zake na kuzingatia maslaha na natija kisha wakabiliane na *fitna* hii kwa kunyamaza, na nyingine kwa kuirudi kwa dalili nzito zitakazoikomesha bila ya kuitaja, na nyingine kwa kusimama imara dhidi yake na kuitaja. Wakati wa makabiliano yafaa akili ya da'wa kuwa na makini na kupima ili isizidishe chochote kwani kufanya hivi itakuwa inapoteza juhudi zake na kuangukia walipotaka wenye shari; kupoteza wakati na juhudi zake na kuichosha da'wa na kunyonya nguvu zake kisha wafurahie kuhadaika kwake na kuandaa vishawishi vingine ili waendelee na mchezo wao wanavyotaka.

**88. Wakati duni ni bora**

Maoni ya wanachuoni katika vitabu vya *fikihi* na da’wa yanatofautiana na watu; wanafadhilisha kauli moja juu ya nyingine. Kufadhilisha kauli fulani hutegemea fahamu za watu, hali zinazowakabili na kiwango cha elimu yao. Sio katika hekima kulazimisha watu kuifuata rai fulani hata ikiwa mtu anaitakidi rai aliyonayo ni sahihi na bora kuliko rai waliyonayo wenzake. Ni bora kuafikiana na kuwa na umoja katika rai na kauli ya sawa kuliko kutofautiana na kukatana katika kauli au rai ipi ndiyo bora zaidi. Kushirikiana katika rai iliyo duni ni bora kuliko kugombana katika rai iliyo bora.

**89. Kulingania Umma**

Kulingania Umma (jumla ya watu) kunahitaji kuzungumzia misingi ya dini ambayo imekubalika na maimamu wote na kujiepusha na hitilafu mbali mbali za wanachuoni au zaidi ya hitilafu hizo kusimulia misimamo, hadithi, tafsiri na hukumu zisizokubalika au kuwaingiza katika masuala kwa mgawanyiko wake katika vitabu vya *fikihi* na masuala ya nadharia pekee; ‘ikiwa kadha itakuwa kadha’, yanayoweza kutokea na yasiyoweza kupatikana. Mazungumzo kama haya yana mahala pake maalum, na wanaoyazungumzia wana misingi na mipaka ambayo hawaivuki. Ama jumla ya watu na wanafunzi wachanga wafaa kushughulishwa kwa mambo watakayonufaika nayo katika maisha yao na wanayohitajia katika maisha ya kila siku.

**90. Kuzingatia hali na wakati**

Kuwapenda ulamaa wema wenye ikhlasi ni wajibu juu ya kila Mwislamu, waliotangulia na walioko na kuwaombea dua na kuchukua mfano mwema kutoka kwao. Lakini haifai kwa hali yoyote kuwatukuza na haifai pia kuchukua tajriba zao na misimamo yao bila ya kuzingatia hali mahususi na wakati maalum walioishi. Tunawajibika kujitahidi kuzingatia hali na wakati wetu ili tupate mwongozo utakao ambatana na hali na wakati wetu kama walivyofanya wao.

**91. Ada sio dini**

Katika zama fulani, baadhi ya ada, desturi na mazowea huwa ni mzigo kwa kuonekana ni miongoni mwa mafunzo ya dini ilhali sio dini. Ada hizi hujitokeza sana katika hafla kama vile ndoa na matangamano mbalimbali katika jamii kama vile kifo na hasa kumuhusu mwanamke. Kwa hivyo yatupasa kutofautisha baina ya ada na dini na tuzikubali ada au kuzikataa kwa misingi ya dini.

### 92. Muumini mwenye uwezo

Ni jukumu letu kulea na kuwaandaa waumini wenye nguvu kwa sababu muumini mwenye uwezo ni bora na anapendwa na Allah kuliko muumini aliye dhaifu au hana uwezo, kwa mujibu wa hadithi sahihi. Nguvu hizi zapatikana katika usahihi wa akida, uthabiti wa imani, uzuri wa tabia na mwenendo, na kupevuka kwa akili. Kulingana na haya, yafaa kuhifadhi miili na siha yetu kamili, kwa kuimarisha lishe bora, kufanya mazowezi ya mwili, usafi na kadhalika na kutahadhari na vyote vinavyodhuru afya kama madawa ya kulevya, sigara, pombe na kadhalika. Kufanya hivi kuna faida kubwa; miongoni mwa faida hizi ni uwezo wa kuhimili uzito wa da'wa kwa hima na uweza.

## Tamati

Umoja wa madola ya Sovieti ulianguka tangu miongo miwili iliyopita na mfumo wa ubepari wa kimagharibi unapitia wakati mgumu kwa mitihani mikubwa. Misingi mikubwa ya ubepari wa nchi za maghribi iliyokubalika imetetemeshwa na leo nguzo zake msingi zimekuwa suala la shaka na kuregelewa. Leo, ni dhahiri kuwa hali iliyoleta nguvu na uwezo mkubwa wa nchi hizi na kufaulu kwa miaka mingi imeanza kudorora na sababu za kuporomoka zinajitokeza kila kukicha na Sunna za Allah aliyetukuka hazichelewi wala kubagua yeyote.

Hakuna mjuzi wala hodari aliyebakia katika ardhi hii anayeweza kuokoa wanadamu isipokuwa nyinyi walinganizi wa Uislamu, basi munawajibika muwe na mustawa unaofaa katika dini na kuelewa vyema hali wakati mnaoishi ili muwe rubani wa safina hii ya da’wa. Mukinfanya hivyo mutajinufaisha na kuwanufaisha walimwengu; Waislamu na wasio kuwa Waislamu.

Jumla ya wajibu wenu unaendelea zama zote, mahala popote na kulenga watu wote, na ulinganizi wenu ni mwito wa huruma, sheria ya wepesi yenye kuondoa dhiki na uzito, na kuhurumia walimwengu wote na kwa sababu hakuna budi kuelewa wajibu na jukumu lenu vizuri na muelewe kuwa nyinyi na walinganizi sio makadhi, warekebishaji sio wachochezi, wajenzi sio waharibifu, wenye huruma sio wenye chuki, kazi yenu inafaa kuwa kama anavyokuwa baba mlezi na watoto wake, au tabibu anapomhudumuia mgonjwa wake sio kazi ya mlinda jela na mfungwa ambaye anaadhibu wala ya aliyedhulumiwa analipiza kisasi.

Mukijipamba na sifa hizi mutakuwa viongozi walio ongoka na kuwanufaisha zaidi waja wa Allah. Viumbe vyote ni waja wa Allah, na anayependwa zaidi na mbora kwa Allah ni yule anayewanufaisha waja wa Allah zaidi. Mkifikia daraja hii watu – kwa mapenzi yao – watawapa uongozi muwaongoze katika heri na nuru ya Uislamu.

Nyaraka hizi zimekusanya jumla ya misingi iliyopendekezwa ambayo ni matunda ya tajriba ya muda mrefu, masomo yakuendelea, kuzingatia kwa kina, na dhiki, tajriba na ufuatiliaji wa matukio na hali ya Waislamu. Makusudio yake ni ziwekwe nyaraka hizi mbele ya Waislamu kwa jumla na wenye busara hasa ili ziwe mkataba na mpangilio wa kazi ya da’wa, na nidhamu ya mawazo na utendakazi ili kuongeza masikizano, usawa, na utendakazi na kupunguza hitilafu, makosa na uzembe baina ya walinganizi.

Yatarajiwa nyaraka hizi zitapokelewa na walinganizi na kusomwa kwa makini na kuongeza rai au kupunguza na kurekebisha au kuongeza.

Tunaahidi watakao tuandikia kuwa maoni yao yatapokelewa na kupewa umuhimu ufaao na tunawaomba wahisi maoni ya nyaraka hizi ni yao wao wenyewe basi waandike chochote wanachoona kitanufaisha da’wa na kuwasaidia Waislamu, Allah awalipe na twawashukuru.

Hakika kutoa maoni mchana na kuyajadili wazi ni njia bora ya kutambua makosa na usawa uliomo, kutokana na fikra hii ya kuhamasisha hima ya walinganizi ili faida ipatikane kwa rai zao, kwa lengo la kuboresha yaliyomo katika nyaraka hizi na kuwa karibu zaidi na ukamilifu na kupokelewa na taasisi na vyama vya Kiislamu. Nyaraka hizi ni zawadi kwa vyama na

taasisi hizi; kila chama na taasisi ichukuwe yale yanayoambatana na hali yake na kuongeza mengine katika hayo au kuboresha watakayofaidika nayo. Kufanya hivi kutaleta heri nyingi kwa idhini ya Allah aliye na uwezo na utukufu.

Usaidizi na taufiki yatoka kwa Allah, twamuomba Allah atuafikishe kwa yale anayoridhia na atutumie katika taa yake, hakika Yeye ni muweza wa kila jambo.

Fikra hii ya Mkataba na mwito kwa Waislamu kwa jumla na walinganizi miongoni mwao hasa kukusanyika na kuungana katika misingi, misimamo na miondoko ambayo inabuni mkataba adhimu wa kazi ya kulingania, na mpangilio na mfumo wa mawazo ya utendakazi ili ipanuke mipaka ya kuamiliana na kushirikiana baina ya walinganizi na kuzidisha usawa na nishati katika da'wa na pia vilevile kupunguza mipaka ya hitilafu na kutofautiana, na kupunguza makosa na kuondoa uzembe.

Mkataba huu unanuia kueneza roho ya mahaba na kuaminiana baina ya walinganizi, kuleta undugu na umoja, na kushajiisha roho ya kukosoana kwa wema na kuongeza njia za mazingatio na fikira. Pia unawania kuleta uvumbuzi na njia mpya za kufikiria na ushirikiano katika yale tunayoafikiana na kusameheana katika yale tunayotofautiana kwayo na unahimiza kutoka katika duara la uzembe kuenda katika duara la utendakazi.

Mkataba huu unakusudia kuwa muelekeo wa kazi unaotokana na Qur'ani na Sunna mbali na kukia mipaka ya dini au kuipuuza na kuwa mfano wa wastani na uadilifu; haubebi nembo za kundi fulani, au mkusanyiko maalum au mfumo wa chuo cha da'wa mahususi, au jitihadi ya *kifikihi*, au kulemea mawazo ya nchi fulani; na mkataba huu haulengi kusaidia wala kupinga upande wowote.